**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA PILI**

**Kikao cha Tisa - Tarehe 17 Februari, 2006**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati ifuatayo iliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:**

Taarifa ya mwaka ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2004.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 94

**Uwekaji wa Lami Barabara ya Kigogo - Mabibo - Mandela - Tabata**

**MHE. HALIMA J. MDEE** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuweka lami kwenye barabara ya Kigogo-Mabibo hadi barabara ya Mandela kuelekea Tabata ili kupunguza msongamano wa magari katika barabara ya Morogoro?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Halima Mdee, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Kigogo - Mabibo- Mandela kuelekea Tabata ni barabara ya mjini yaani *urban road* na inahudumiwa na Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni. Barabara hii ni muungano wa barabara tatu ambazo ni Kigogo - Mabibo, Mabibo - Mandela na Mandela - Tabata. Barabara hii imekuwa ikifanyiwa matengenezo ya mara kwa mara na Manispaa ya Kinondoni. Kwa mwaka 2005/2006 jumla ya shilingi 9,836,000 zilitumika kuweka kifusi kwenye sehemu korofi na kuichonga kwa greda.

Mheshimiwa Spika, barabara hii inapitika isipokuwa katika mpaka wa Manispaa za Kinondoni na Ilala eneo la Tabata ambapo pana mkondo wa maji na hakuna daraja. Eneo hilo hupitika wakati wa kiangazi tu. Kwa kuwa sehemu hii ipo mpakani mwa Halmashauri za Manispaa za Ilala na Kinondoni, mawasiliano yanaendelea kufanywa kati ya Manispaa hizi mbili ili waunganishe nguvu na kujenga daraja kwa pamoja.

Mheshimiwa Spika, mzunguko wa barabara hii uliotajwa hapo juu hauna mahali unapokutana moja kwa moja na barabara ya Morogoro. Hata hivyo kujengwa kwa barabara hiyo hakutapunguza msongamano wa magari katika barabara ya Morogoro. Ili kupunguza msongamano inabidi kipande cha barabara ya Kigogo - Maziwa kinachoanzia eneo la Shungashunga hadi *TANESCO* Ubungo kwenye makutano ya barabara ya Morogoro nacho kijengwe. Kwa kufanya hivyo gharama ya kujenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami inagharimu kiasi cha shilingi 2,975,310,000 na gharama ya kujenga barabara iliyotajwa hapo juu ya kilometa 7.8 ni shilingi 2,550, 265,741.

Mheshimiwa Spika, katika jitihada za kuiboresha barabara hiyo Manispaa ya Kinondoni ilikuwa ikishirikiana na wahisani hasa *Tanzania Japan Food Aid Counterpart Fund* imegharamia ujenzi wa *box culvert* la Kigogo baada ya lile lililokuwepo kuvunjika. Mradi huo uligharimu kiasi cha shilingi 229,344,000. Aidha, Manispaa imefanya juhudi ya kununua mitambo ya matengenezo ya barabara yenye thamani ya *US Dollar* 950,000 kwa mkopo ambao kwa sasa hivi mkopo huu unaendelea kulipwa kwa awamu. Kwa kutumia mitambo hii Manispaa imeweza kuchonga na kuiwekea kifusi barabara hii pamoja na kuchimda mifereji.

Mheshimiwa Spika, kutokana na ufinyu wa Bajeti Manispaa ya Kinondoni haina mpango wowote wa kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami kwa sasa.

Na. 95

**Maporomoko ya Mawe Katika Mlima Kilimanjaro**

**MHE. LUCY J. OWENYA** aliuliza:-

Kwa kuwa hivi karibuni kulitokea maafa katika Mlima Kilimanjaro yaliyosababishwa na kuporomoka kwa mawe na majabali yaliyowaua watalii pamoja na watu kadhaa kuumia:-

(a) Je, tukio hilo linaashiria nini ikilinganishwa na utabiri uliofanywa na baadhi ya wataalam kuhusu kuondoka kwa barafu iliyo juu ya Mlima huo?

(b) Je, ni nini hatma ya upatikanaji wa maji ya kuaminika kwa wananchi waishio Kilimanjaro ikiwa barafu hiyo itaendelea kuyeyuka?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MAZINGIRA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla sijajibu swali la Mheshimiwa Lucy Owenya, Mbunge wa Viti Maalum, napenda kutoa maelezo mafupi ya awali kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tarehe 4 Januari, 2006 saa 3.30 asubuhi kulitokea maafa ya wapandaji Mlima Kilimanjaro yaliyosababishwa na kuporomoka kwa mawe na majabali.

Mheshimiwa Spika, kulingana na maelezo yaliyopatikana kutoka katika eneo la tukio ni kwamba muda mfupi kabla ya ajali, mawe yaliporomoka kutoka ukingo wa shimo lililo kwenye kilele cha Mlima Kilimanjaro. Wapandaji hao walijikuta wakipishana na mawe makubwa yakiporomoka kwa kasi.

Kwa mujibu wa taarifa tuliyoipata kutoka Mamlaka ya Hifadhi ya Mlima Kilimanjaro *(KINAPA),* watalii watatu kutoka Marekani walifariki papo hapo na wengine watano walijeruhiwa, wanne raia wa Marekani na mmoja akiwa Mtanzania, tunamwomba Mwenyezi Mungu azirehemu roho za marehemu. *Amin.*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Lucy Owenya, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Hadi sasa chazo cha maporomoko ya mawe katika Mlima Kilimanjaro hakijajulikana, lakini kuna uwezekano wa mojawapo ya sababu mbili zifuatazo:-

(i) Kuendalea kupungua kwa barafu mlimani kutokana na kuongezeka kwa joto duniani.

(ii) Nguvu za kijiolojia ndani ya Mlima ndizo zilizosababisha kuporomoka kwa mawe hayo. Mlima Kilimanjaro kama tunavyojua ni *Volcano* iliyotulia kwa muda mrefu yaani *dormant volcano*.

(b) Mtafiti Jacques Blot wa Chuo Kikuu cha Bordeaux, Ufaransa anaripoti kwamba tangu mwaka 1912 mpaka sasa theruji ya Mlima Kilimanjaro imepungua kwa zaidi ya asilimia 80. Utafiti uliofanyika mwaka 1999 na 2000 na Dr. Lonnie Thompson wa Chuo Kikuu cha Ohio, Marekani akishirikiana na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, ulionyesha kwamba theluji ya Mlima Kilimanjaro haitaweza kudumu zaidi ya miaka 15 ijayo kuanzia mwaka 2000. Ripoti ya utafiti huu inaonyesha kwamba theluji ya Mlima Kilimanjaro sio tu inapungua kina bali hata kwa upana.

Kwa kuwa kuyeyuka kwa theluji ya Mlima Kilimanjaro kunatokana na ongezeko la joto duniani ni dhahiri kwamba ongezeko hilo litasababisha hali ya hewa, ikolojia ya Mlima, upatikanaji wa mvua na hivyo kuathiri vyanzo vya maji. Hata hivyo mfumo mzima wa mvua na upatikanaji maji Kilimanjaro una uhusiano mkubwa na uoto wa asili kando ya mlima. Vyanzo vya maji vinapungua jinsi watu wanavyoharibu uoto huo.

Mheshimiwa Spika, ili upatikanaji wa maji kwa wananchi waishio Kilimanjaro na sehemu nyingine nchini uwe wa kuaminika, inatubidi tuchukue hatua zifuatazo:-

(i) Kudhibiti ukataji miti katika msitu.

(ii) Kuongeza kasi ya upandaji, ukuzaji na utunzaji wa miti.

(iii) Kudhibiti uchomaji wa misitu na mbuga.

(iv) Kupanda miti ya asili katika sehemu zilizo kando ya mito.

(v) Halmashauri za Wilaya kutambua, kumiliki, kuhifadhi na kulinda vyanzo vya maji.

Na. 96

**Viwanja vya Michezo**

**MHE. DIANA M. CHILOLO (k.n.y. MHE. MGANA I. MSINDAI)** aliuliza:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa viwanja vya michezo vya Kirumba - Mwanza, Ali Hassan Mwinyi - Tabora, Namfua - Singida, Samora Machel - Iringa na kadhalika vinavyomilikiwa na Chama cha Mapinduzi havijakamilika na kiwanja cha Iringa kiliezuliwa paa lake na upepo na mpaka sasa hakuna mipango wa kurudisha paa lake kwa ukosefu wa fedha.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuvikamilisha viwanja hivyo ili viweze kutumika kwa michezo ya ndani na nje?

(b) Je, Serikali iko tayari kutafuta wafadhili ili waviendeshe kwa ubia?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO (MHE. JOEL N. BENDERA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mgana Msindai, Mbunge wa Iramba Mashariki, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, viwanja vya michezo vya Kirumba - Mwanza, Ali Hassan Mwinyi - Tabora, Namfua - Singida, Samora Machel - Iringa na kadhalika vinamilikiwa

na Chama cha Mapinduzi. Kwa hiyo, ni mali ya CCM. Baadhi ya viwanja vya Wilaya na Mikoa vinamilikiwa na Halmashauri husika na taasisi mbalimbali hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, viwanja alivyovitaja Mheshimiwa Mgana Msindai ni kweli baadhi havijakamilika. Kwa ajili ya kuvikamilisha viwanja hivyo, Serikali imeshauri mamlaka husika kuvikamilisha na vingine kuvikarabati ili viweze kuwa na viwango vya Kimataifa, vitakavyowezesha michezo ya Kitaifa na Kimataifa kuchezwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuingia ubia na makampuni au watu binafsi, wamiliki wa viwanja hivi wakitaka ushauri Serikali itakuwa tayari kutoa msaada unaohitajika. *(Makofi)*

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, je, Serikali haioni kwamba kuna kila sababu yenyewe kuingia ubia na Chama cha Mapinduzi ili kukamilisha viwanja hivi na kuanza kugawana mapato kwa maslahi ya Watanzania?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO (MHE. JOEL N. BENDERA):** Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu kwenye swali la msingi, viwanja vingi hapa nchini vinamilikiwa na taasisi mbalimbali ikiwemo Chama cha Mapinduzi na kama nilivyosema Serikali haina tatizo lolote la kuingia ubia na wahusika hao. Kinachotakiwa ni kwamba wao kama wanahitaji watuletee maombi ili tushirikiane nao katika kutafuta wafadhili. *(Makofi)*

**MHE. SHOKA KHAMIS JUMA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali dogo la nyongeza. Hivi viwanja kwa nini vimilikiwe na Chama cha Mapinduzi?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO (MHE. JOEL N. BENDERA):** Mheshimiwa Spika, Chama cha Mapinduzi katika Ilani yake ya Uchaguzi imehamasisha maendeleo ya michezo nchini na katika utaratibu ni kwamba chama chochote kinaruhusiwa kufanya kama ambavyo Chama cha Mapinduzi kimefanya. Viwanja hivi ni binafsi, wao ndiyo waliohamasisha wananchi kujenga kama vile ambavyo wewe kama unataka kufanya shughuli yako yoyote, unahamasisha wananchi, unataka kujenga shule, unataka kujenga zahanati, unahamasisha wananchi. Chama cha Mapinduzi kimetafuta hati miliki, kimehamasisha wanachi kikajenga viwanja. *(Makofi)*

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, kwanza nampongeza kwa majibu mazuri na nikipongeze Chama cha Mapinduzi kwa kumiliki viwanja.

Swali langu ni kwamba kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amekubali kwamba Serikali haina tatizo la kuingia ubia na mamlaka inayomiliki viwanja hivi na kwa kuwa Rais Mstaafu wa Awamu ya Tatu, Mheshimiwa Benjamin Mkapa amefanya kazi nzuri ya kutuachia wanamichezo kiwanja kizuri cha kisasa cha Kimataifa.

Je, Serikali haioni kwamba iko haja kwa dhana ile ile ya kuingia ubia na mamlaka hasa kwa ajili ya kiwanja cha Kirumba ili kitengenezwe kiwe kina hadhi ya Kimataifa kama vile cha Dar es Salaam ili kitupe fursa sisi Watanzania kuweza kuomba kuandaa mashindano ya Kimataifa?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO (MHE. JOEL N. BENDERA):** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema, hatuna tatizo lolote la kuendeleza viwanja vingine. Sasa hivi Serikali Bajeti yake imejikita kutengeneza kiwanja cha Ngamani cha Dar es Salaam yaani *Complex Stadium*.

Mheshimiwa Spika, nia ya Serikali baada ya kumaliza kiwanja hicho tutaendelea kujenga viwanja vingine katika Mikoa.

Na. 97

**Soko la Kimataifa la Laela**

**MHE. PAUL P. KIMITI (k.n.y. MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA)** aliuliza:-

Kwa kuwa Mji Mdogo wa Laela ni kituo muhimu sana kwa biashara, je, Serikali inaweza kujenga Soko la Kimataifa Laela ili kukuza biashara na uchumi wa Laela na Wilaya nzima ya Sumbawanga?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya, Mbunge wa Kwela, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inakubaliana na pendekezo la Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya, kuwa ujenzi wa Soko la Kimataifa katika Mji Mdogo wa Laela utakuza biashara na uchumi wa Laela na Wilaya nzima ya Sumbawanga. Hata hivyo, ili kufanikisha ujenzi wa soko hilo mambo yafuatayo hayana budi kufanyika:-

(i) Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga Vijijini kuonyesha dhamira hiyo kwa kutoa kipaumbele katika mpango wake wa maendeleo wa kujenga soko katika Mji Mdogo wa Laela. Dhamira hii ni muhimu ili kuwezesha maandalizi ya mfumo wa umiliki na uendeshaji wa soko.

(ii) Kufanya tathmini ya kina ya mahitaji ya soko linalopendekezwa kujengwa.

Mheshimiwa Spika, ili kufanikisha ujenzi wa Soko la Kimataifa katika Mji Mdogo wa Laela pamoja na maeneo mengine nchini, Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko, kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya itafanya tathmini ya maeneo muhimu *(strategic areas)* yanayofaa kujengwa Masoko ya Kimataifa kama lile la Kibaigwa ambalo lilligharimu takriban shilingi milioni 400.

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kunipa nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, napenda kuuliza maswali yafuatayo:-

Kwa kuwa Halmashauri ya Wilaya imeshapeleka mapendekezo yake ya kuomba msaada wa Serikali Kuu ili angalau kituo hicho kijengwe. Je, Mheshimiwa Waziri atakubaliana nami ya kwamba kwa sababu mwaka jana peke yake Laela iliweza kuzalisha zaidi ya tani 10,000 na kushindwa kupata soko la uhakika kutokana ka kukosa soko lenyewe?

La pili, je, ni misingi ipi iliyotumika Kibaigwa kufanywa liwe ni Soko la Kimataifa wakati Laela inashindwa kupewa hadhi ya namna hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, vigezo ambavyo vinatumika ili kuweza kujua kwamba sehemu inafaa kujengwa au la ni hivi vifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza inabidi kujua ni aina gani na kiasi gani cha mazao ambayo yatauzwa katika soko hilo

Pili ni muhimu vile vile kujua kwamba ni maeneo gani ambayo yatahudumiwa na hilo soko likijengwa yaani *catchment area*. Lakini vile vile ni muhimu kujua miundombinu mingine ambayo ipo katika maeneo ya hilo soko. Pia ni vyema kujua ujenzi wa soko utagharimu kiasi gani kwa sababu sasa hivi katika hii programu ya *AMSDP* gharama ya ujenzi wa soko moja ni milioni 150.

Mheshimiwa Spika, ni vema kujua athari ambazo zitaleta madhara baada ya soko hilo kujengwa, kwa mfano *sewerage system* ili ziweze kuchukuliwa hatua mapema kabla ya soko hilo kujengwa. Lakini ni vema kujua ukubwa wa eneo ambalo soko linatarajiwa kujengwa kwa sababu *size* ya chini ya kujenga soko ni heka nne. Kwa hiyo, mambo hayo lazima yazingaitwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile ni vema kujua kama kuna maghala au mawasiliano yoyote ambayo yangeweza kufanya biashara iwe rahisi zaidi.

**MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa maelezo yanayoeleza kijiji cha Laela kuwekewa Soko la Kimataifa eneo hili linafanana na Ilula, Wilaya ya Kilolo ambako kunazalishwa matunda kwa wingi na pia mazao yanayotoka eneo la Dabaga.

Je, Ilula pia itakuwa kwenye mpango wa kuweza kujengwa soko la Kimataifa ili matunda yaweze kuuzwa kwa urahisi badala ya kutengemea kupelekwa Dar es Salaam?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, katika mpango huu wa *AMSDP* ni Wilaya 20 tu ambazo zinaweza kujengwa masoko kati ya Wilaya 38 za Mikoa minane. *(Makofi)*

Kwa hiyo, kwa kutumia vigezo hivyo hivyo na kwa kupata wafadhili wengine, Serikali inaweza kuwasiliana na Halmashauri kwa ajili ya kufanya tathmini kwa kutumia vigezo hivyo hivyo ili tuone kama eneo hilo linafaa kujengwa soko.

Na. 98

**Maeneo ya Uchimbaji Almasi Mwadui**

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED** aliuliza:-

Kwa kuwa mwaka 2004/2005 Serikali ilikuwa na mpango wa kuwapimia maeneo ya uchimbaji wa almasi wadogo wa mgodi wa Mwadui:-

(a) Je, ni wachimbaji wangapi waliostahili kupimiwa viwanja?

(b) Je, ni wangapi waliokwishapimiwa na kukabidhiwa hati zao?

(c) Je, mkataba wa Serikali na *Williamson Diamonds* utaisha lini na je, Serikali ina mpango gani wa kuuza hisa zake zilizosalia?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mbunge wa Wawi, napenda nitoe maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tarehe 4 Desemba, 2003, Waziri wa Nishati na Madini akiwa Maganzo, Shinyanga aliongea na wachimbaji wadogo wa almasi wa eneo hilo na kuwaahidi kuwaondolea kero ya kutokana na viwanja walivyomilikishwa kihalali. Katika kutekeleza ahadi hiyo, Wizara yangu ilitenga eneo la hekta 14,000 kwa tangazo la Serikali *GN* namba 528 la tarehe 3 Desemba, 2004.

Baada ya kutenga eneo hilo na kwa kufuata matakwa ya Kanuni za Madini za mwaka 1999, iliundwa kamati ya kugawa viwanja, Mwenyekiti wa Kamati alikuwa ni Mkuu wa Wilaya ya Kishapu na Wabunge wawili, Mbunge wa Jimbo la Kishapu na Mbunge wa Jimbo la Shinyanga Mjini, walikuwa miongoni mwa wajumbe wa Kamati.

Kamati ilitoa tangazo la kukaribisha maombi ya kumilikishwa eneo tarehe 11 Mei, 2005. Maombi yaliyopokelewa hadi tarehe 24 Juni, 2005, ni 1,045, kati ya hayo maombi 1,043 yamekubaliwa. Maombi mawili yalikataliwa kwa kutotimiza vigezo. Maombi yaliyokubaliwa yamechukuwa eneo la hekta 8,500 kati ya hekta 14,000 zilizotengwa, hekta 5,500 zilizobaki zitagawiwa katika awamu ya pili ya zoezi hilo ambapo tunaendelea kupokea maombi. Katika maombi 1,043 yaliyokubaliwa, ni maombi

504 tu ndiyo waombaji wake wamekamilisha malipo ya ada zote na hivyo leseni zimeandaliwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi, sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, wachimbaji waliostahili kupimiwa viwanja ni wale waliowasilisha maombi yao na kufikia vigezo au sifa za kupewa viwanja.

(b) Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katika utangulizi, maombi 1,043 yamekubaliwa na mawili hayakuwepo *offer* kwa sababu waombaji walichagua eneo ambalo lilishachaguliwa na waombaji waliotangulia. Kati ya maombi 1,043, maombi 504 yamekamilisha ada zinazotakiwa na hati au leseni zimeandaliwa.

(c) Mheshimiwa Spika, mkataba wa umiliki wa mgodi wa *Williamson Diamonds Limited,* ambapo Serikali inamiliki hisa asilimia 25 na kampuni ya *Wilcroft* ya Afrika Kusini hisa asilimia 75 hauna mwisho, mwisho wake ni hapo mashapo ya mgodi yatakapomalizika na mgodi kufungwa au Serikali itakapoamua kuuza hisa zake. Hivi sasa Serikali haina mpango wa kuuza hisa zake.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Spika kwanza namshukuru sana Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri, nina maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwa kuwa tatizo moja la wachimbaji wadogo wadogo si tu kupewa viwanja ni pamoja na zana za kufanyia kazi za kuchimbia. Je, Serikali ina mpango gani wa kuweza kuwapatia vifaa vya kuweza kuchimbia katika maeneo ambayo tayari wameshapimiwa?

Pili, kwa kuwa juzi tulipitisha sheria ya Muswaada wa *SEZ* ambapo Serikali kwa njia moja ambayo inataka kufanya ni kuweza kutumia rasilimali za nchi kuongeza mapato. Eneo moja ambalo lingeweza kutupatia mapato ya haraka ambayo tunayakosa hivi sasa ni usafirishaji wa almasi zinazokwenda nje zikiwa ghafi. Je, Serikali itakuwa tayari kupiga marufuku usafirishaji wa almasi ghafi nje pindi atakapopatikana mwekezaji wa kujenga kiwanda cha kusafirisha almasi katika maeneo ya *SEZ?*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, Serikali hivi sasa ina mkakati wa kuboresha mazingira kwa ajili ya wachimbaji wadogo wadogo katika nchi nzima si sehemu ya almasi peke yake. Kwa hivi sasa tumeshaanza mkakati kwa kutumia shirika la *STAMICO* kuunda sera mpya ya kuweza kuwasaida hawa wachimbaji wadogo wadogo kwa kuwapatia zana na vifaa vingine.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la usafirishaji wa almasi ghafi nje ya nchi, tayari Serikali ilshabadilisha sheria kuhusu *royalties* ambazo zinalipwa ili ku-*encourage* wachimbaji wapeleke almasi na madini mengine nje yakiwa *finished product* kwa kubadilisha ile *royalties* asilimia tatu kwa tano kwa ajili ya *unpolished* na *uncut* na zile ambazo zinatoka *polished* na *cut royalties* ni *zero rated. (Makofi)*

**MHE. FRED M. TUNGU:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, naomba kuuliza swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005, imeahidi kwa wananchi wanaoishi karibu na migodi Serikali itaweka mipango ya makusudi kuwanufaisha wananchi hao. Je, Serikali ina mpango gani kwa wananchi wanaoishi kijiji cha Songwa, Utemini, Idukilo na Uchambi ili nao wanufaike na mgodi wa almasi wa Mwadui ambao umekuwa ukichimbwa almasi kwa muda mrefu kama vile wananchi wa Ngorongoro wanavyonufaika na utalii katika maeneo yao?

**SPIKA:** Nadhani Mheshimiwa hili pengine tutapata faida zaidi likiulizwa kama swali la pekee. *(Makofi)*

**MHE. PHILEMON NDESAMBURO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Hapo awali tulikuwa na kiwanda cha kusafisha Almasi kule Iringa na kilikuwa kinasafisha Almasi yetu kabla haijapelekwa nje. Nini hatma ya kile kiwanda, kwa nini kilifungwa na sasa hakipo tena?

**SPIKA:** Naona hili nalo ni swali ambalo ni jipya kabisa, lakini kama Waziri anataka kujibu. Basi Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Philemon Ndesamburo, kama ifuatavyo:-

Suala la biashara ya usanifu au ukataji limekuwa likiendana na mwenendo mzima wa biashara ya madini hayo. Huko nyuma ilionekana kwamba shughuli hii kuendelea kufanyika hapa nchini pengine haikuwa na manufaa zaidi kwa wale wawekezaji kama ambavyo ingefanyika sehemu nyingine. Lakini napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inatambua umuhimu wa kurejesha usanifu wa vito hivi hapa nchini na kama ambavyo Mheshimiwa Naibu Waziri amejibu vizuri sana kwamba hapa hapa Bungeni tulishapitisha marekebisho ya sheria ya kuhakikisha kwamba madini ya vito yanasanifiwa hapa nchini na ni mkakati wa Serikali kuhakikisha kwamba madini yetu yanaongezewa thamani na yanauzwa nje yakiwa yamesanifiwa, na ndivyo ilivyo katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi Ibara ya 38 na 39. *(Makofi)*

Na. 99

**Makato ya Fedha ya Polisi Wastaafu**

**MHE. ETHERINA J. KILASI (k.n.y. MHE. BENSON M. MPESYA)** aliuliza:-

Kwa kuwa polisi wengi waliostaafu walikatwa fedha kwa ajili ya pensheni zao na Mkuu wa Jeshi la Polisi na baada ya kustaafu, polisi hao wamekuwa wakidai hizo fedha bila mafanikio:-

Je, ni lini askari hao watapatiwa malipo hayo?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Benson M. Mpesya, Mbunge wa Mbeya Mjini, naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, mtumishi wa umma ili aweze kulipwa mafao yake ya pensheni ni lazima akamilishe mambo yafuatayo:-

(i) Barua yake ya ajira ya kwanza.

(ii) Barua yake ya kuajiriwa katika masharti ya kudumu na malipo ya uzeeni.

(iii) Barua ya kuthibitishwa kazini.
(iv) Barua iliyompandisha cheo cha mwisho ambacho amestaafu nacho.

(v) *Salary Slip* ya miezi michache kabla ya kufikia tarehe ya kustaafu.

(vi) Barua ya mwajiri ya kumkubalia kustaafu kwake.

(vii) Nakala ya makato yake ya pensheni ambayo huandaliwa na mwajiri.

Mheshimiwa Spika, haya yote yanapokuwa yamekamilika katika wakati unaotakiwa ambayo ni miezi sita kabla ya tarehe ya kustaafu, basi mtumishi husika huweza kulipwa mafao yake mapema bila usumbufu wowote.

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa makato ya michango ya mafao ya kuchangia pensheni kwa watumishi hufanywa kupitia mishahara ya kila mwezi ya watumishi na fedha hizo hutunzwa Hazina, Shirika la Taifa la Hifadhi za Jamii na Mfuko wa Pensheni wa Watumishi wa Umma. Michango hiyo ya Watumishi haitunzwi na mwajiri.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi, naomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa Benson M. Mpesya, Mbunge wa Mbeya Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, askari polisi wote ambao wamestaafu kazi na walitimiza masharti ya msingi ambayo nimeyataja katika maelezo ya utangulizi, wameihalipwa mafao yao ya pensheni. Malipo ya pensheni huchukua muda mfupi iwapo nyaraka zote muhimu zinakuwemo ndani ya jalada la mtumishi.

Mheshimiwa Spika, kuna uwezekano kwamba wapo askari ambao bado hawajalipwa pensheni yao, basi hao ni sehemu ya wale ambao kumbukumbu zao za utumishi hazijakamilika.

Mheshimiwa Spika, kupitia Bunge lako Tukufu, napenda kutoa wito kwa askari wastaafu ambao hawajalipwa pensheni zao wawasiliane na ofisi za makamanda wa Mikoa au ofisi ya Inspekta Jenerali wa Polisi ili kujua tatizo lao liko wapi na hatimaye askari hao waweze kulipwa mafao yao ambayo ni haki yao ya msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, kwa wale askari ambao bado wako kazini, napenda kuwakumbusha watunze kumbukumbu zao za ajira ili kuondoa usumbufu wakati wao wa kustaafu unapowadia.

**MHE. ESTHERINA J. KILASI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali la nyongeza.

Kwa kuwa askari hawa wa Mbeya ambao wamestaafu mwaka 2004 mwezi Juni, inaonyeshwa makato yao yalikatwa na mwajiri lakini hakuweza kuwasilisha mahali ambapo panahusika na kwa kuwa utaratibu wa Serikali kwa siku za huko nyuma pale ambapo Taasisi ya Serikali kama vile Mashirika ya Umma na Taasisi zingine za Serikali ziliposhindwa kuwasilisha makato ya wafanya kazi ambao wamekatwa, kulikuwa na utaratibu wa kuwalipia makato ambayo hayakuwasilishwa ili hao watu ambao wamekatwa wasiweze kuathirika na maisha na baadaye kuweza kumshughulikia yule ambaye hakuwasilisha makato hayo.

Je, kwa nini sasa Serikali isifanye jitihada zozote za kuhakikisha kwamba hawa wafanyakazi wanalipiwa hayo mafao ambayo hayakufikishwa na walipwe pensheni zao badala ya kuishi maisha ambayo wanaishi kwa sasa?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi kwamba wale wote ambao wamekamilisha taratibu ndio ambao wamepata kulipwa malipo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na hao wafanyakazi ambao anawasema Mheshimiwa Estherina Kilasi, Wizara yetu haina taarifa ya suala hilo na kama wapo watu hao tunawaita kama tulivyotoa tangazo kwamba waje tuzungumze ili tukamilishe utaratibu waweze kupata malipo yao. *(Makofi)*

**MHE. ROSEMARY K. KIRIGINI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Napenda kuuliza swali moja dogo tu la nyongeza. Miongoni mwa hao askari ambao wanaodai pensheni wapo baadhi yao ambao wamefariki dunia, je, utaratibu hapa unakuwaje? Ni nyaraka zipi ambazo ndugu zao wanatakiwa wawasilishe kwa Wizara husika ili waweze kupewa malipo hayo? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Spika, kwa wale ambao wamefiwa na mfanyakazi wa Jeshi la Polisi, wanahitaji kupata mambo yafuatayo:-

(i) Kuwa na nakala halisi ya cheti cha kifo.

(ii) Muhtasari wa kikao cha familia cha kumteua msimamizi wa mirathi iwapo marehemu hakuacha wosia.

(iii) Barua ya Mahakama ya kuthibitisha uteuzi wa msimamizi wa mirathi.

(iv) Nakala ya vyeti vya kuzaliwa vya watoto wa marehemu na picha zao.

(v) Nakala ya cheti cha ndoa na picha ya mke ama mume.

(vi) Picha za msimamizi wa mirathi kama msimamizi si mmoja kati ya wanandoa.

Na. 100

**Mradi wa Upatikanaji wa Pembejeo kwa Wakulima**

**MHE. GRACE S. KIWELU** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali itaanzisha mradi wa upatikanaji wa pembejeo kwa wakulima:-

(a) Je, Serikali inaweza kueleza idadi ya Wilaya na viwango vya fedha zilizotolewa kusaidia upatikanaji wa pembejeo hizo?

(b) Je, mikopo hiyo ya pembejeo za kilimo inasimamiwa na nani na kwa ngazi ipi?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. CHRISTOPHER K. CHIZA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Grace Sindato Kiwelu, Mbunge wa Viti Maalum, napenda kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali tayari inao Mradi wa Upatikanaji wa Pembejeo kwa kupitia Mfuko wa Pembajeo *(The National Agricultural Input Trust Fund)* ulioanzishwa mwaka 1994 kwa Sheria ya Bunge Na. 9 ya mwaka 1994. Lengo la mfuko ni kutekeleza sera ya Serikali ya kuhakikisha kwamba wakulima wanapata pembejeo za kilimo kwa wakati na kwa bei nafuu kwa kutoa mikopo ya masharti nafuu kwa waagizaji wa pembajeo ili kuwawezesha kugharamia uagizaji na usambazaji wa pembajeo za kilimo, mifugo na zana za kilimo.

Baada ya kutoa maelezo haya ya utangulizi napenda kujibu swali la Mheshimiwa Grace Sindato Kiwelu, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kuanzia msimu wa mwaka 1995/1996 hadi Juni 30,1999, Mfuko wa Pembejeo umetoa mikopo 259 yenye thamani ya shilingi bilioni 5.8 kwa

wasambazaji wa pembajeo za kilimo na mifugo kwenye Wilaya 50. Hata hivyo, kuanzia msimu wa mwaka 1999/2000 hadi 2001/2002, mfuko ulisitisha utoaji wa mikopo kutokana na mikopo kutorejeshwa kwa wakati katika kipindi hicho.

Baada ya kuboresha taratibu za ukopaji na Serikali kuanza kutoa fedha, kati ya mwaka 2002 na 2005, Mfuko wa Pembejeo umetoa mikopo 730 yenye thamani ya shilingi bilioni 14.1 kwenye Wilaya 69 kwa wasambazaji wa pembejeo za kilimo na mifugo, Vyama vya Msingi vya Ushirika wa Akiba na Mikopo *(SACCOS)*.

(b) Mheshimiwa Spika, mikopo ya pembajeo za kilimo husimamiwa na uongozi wa mfuko wa chini ya Bodi ya Wadhamini wa Mfuko katika ngazi ya Taifa. Aidha, katika ngazi ya Wilaya, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya na Afisa Kilimo wa Wilaya wanahusika katika kusimamia mikopo hiyo kwa kuthibitisha kuwa mwombaji anastahili kupewa mkopo husika kabla ya kupitisha maombi yake na kuyawasilisha kwenye mfuko wa pembejeo.

Mheshimiwa Spika, maombi yote yaliyopokelewa yanafanyiwa tathmini na yaliyotimiza masharti yana wasilishwa kwenye Bodi ya Wadhamini. Waombaji walioidhinishwa na Bodi hujulishwa ili kuweza kukamilisha taratibu za kupata mikopo husika. Mfuko wa Pembejeo kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya hufuatilia matumizi ya mikopo pamoja na marejesho yake.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa kuwa pembejeo ni pamoja na dawa ambazo wakulima wa Pamba wanatumia na mpaka hivi sasa wakulima wa Pamba wanakatwa shilingi 15 kwa kilo kwa kila Pamba inayouzwa. Je, Serikali ina mtizamo gani wa kuhakikisha kwamba kama vile inavyotoa ruzuku kwa mbolea, inatoa pia ruzuku ya pembejeo ya dawa hizi kwa wakulima wa Pamba?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. CHRISTOPHER K. CHIZA):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu kama ifuatavyo:-

Kwanza, ruzuku inayotolewa na Serikali kwa mbolea haibagui, ruzuku hii inakwenda Tanzania nzima. Tulianza na Mikoa ile ya Nyanda za Juu Kusini, hatimaye sasa tunatazama Tanzania nzima. Ruzuku katika mbolea hiyo inapofika hata kule kwa wakulima wa Pamba hatusemi wakulima wa Pamba wasichukue. Lakini tukija kwenye dawa, wakulima wa Pamba tayari wao kwa upande ule wanayo *association* yao ya Pamba ambayo sasa hivi inawashughulikia katika matatizo mbalimbali. Lakini kama Mheshimiwa John Cheyo, kama tulivyozungumza kabla, ikiwa kama mnaona kwamba kuna haja ya dawa za Pamba nazo kuwekewa ruzuku, basi naomba mlichanganue jambo hili, muilete Serikalini kama tulivyofanya kwenye mbolea. *(Makofi)*

**MHE. DR. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amejibu vizuri sana maswali aliyoulizwa, mimi napenda tu kuulizia tamko la Serikali kwamba kuna wakulima ambao wamekuwa

wakikatwa fedha yao kama sehemu ya pembejeo wanapouza Pamba yao na mpaka leo hii hawajalipwa hiyo fedha. Je, Serikali inatoa tamko gani kwa hao wanunuzi ambao wamekuwa wakiwakata fedha hiyo kama sehemu ya pembejeo?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. CHRISTOPHER K. CHIZA):** Mheshimiwa Spika, wakulima ambao wanakatwa fedha zao kwa kukatwa na wanunuzi, Serikali hadi sasa haijaletewa malalamiko kama hayo kwamba wakulima sasa wanalalamika.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunaomba Mheshimiwa Mbunge kama kuna malalamiko kwamba wakulima wanalalamikia makato hayo, mimi naamini makato hayo yamefanywa baada ya maafikiano kwamba yana sababu zake.

Mheshimiwa Spika, lakini kama kuna malalamiko kwamba makato hayo yanawanyanyasa wakulima, naomba vile vile Mheshimiwa Mbunge alilete lizungumzwe kwa sababu hakuna suala ambalo halizungumziki. *(Makofi)*

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa katika Mkoa wa Ruvuma, mvua zinanyesha vizuri na wananchi wa Wilaya ya Namtumbo wamelima mazao ya chakula kwa wingi na muda wa kutia mbolea bado haujaisha na mbolea ya ruzuku imeisha na mahitaji bado na Kampuni ya Mbolea ya Taifa *(TFC)* inayo mbolea ya kutosha katika maghala ya Makambako.

Je, Serikali inaweza kupeleka kwa dharura tani 1,000 za mbolea ya ruzuku ili kuokoa mazao hayo ambayo yamestawi vizuri na yaje kusaidia kupunguza hali ya njaa na kupunguza mzigo kwa Serikali?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, naona swali hili ni la dharura inabidi tu ulijibu kwa sababu kuna njaa nchini. *(Kicheko/Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. CHRISTOPHER K. CHIZA):** Mheshimiwa Spika, kwa kweli ni la dharura na lina uzito wake. Naomba nijibu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, fedha za mbolea ya dharura ambazo zimetolewa kama nilivyojibu wakati nikijibu suala la pembejeo, tulisema kwanza, fedha hiyo haitoshi, ni kidogo sana na ndiyo maana nilimjibu Mheshimiwa Mbunge aliyeuliza swali wakati huo kwamba kwa kweli si rahisi kuwafikia wakulima wote kuwapa mbolea kiasi wanachotaka.

Mheshimiwa Spika, lakini kama ulivyosema kwamba suala hili lina unyeti na udharura katika hali hii ya njaa, naomba nijibu kwamba tutalijadili Serikalini, sina majibu sasa hivi ili liweze kupatiwa majibu. *(Makofi)*

Na. 101

**Barabara ya Iringa - Dodoma - Minjingu**

**MHE. PASCHAL C. DEGERA** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali iliahidi kujenga barabara ya Iringa - Dodoma - Minjingu kwa kiwango cha lami na kwamba ilitenga fedha kwa ajili ya kufanya kazi hiyo:-

(a) Je, ni lini kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa barabara hii itaanza?

(b) Je, kazi ya ujenzi wa barabara hiyo kwa kiwango cha lami utaanza lini?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Paschal Degera, Mbunge wa Kondoa Kusini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa barabara ya Iringa - Dodoma na kuendelea hadi Minjingu imegawanyika katika sehemu tatu ambazo ni Dodoma hadi Iringa, Dodoma hadi Babati na Babati hadi Minjingu na utekelezaji wake ni kama ifuatavyo:-

(i) Mheshimiwa Spika, Dodoma - Iringa, Wizara inakamilisha taratibu za kupata kampuni ya kufanya usanifu wa kina wa barabara hii chini ya ufadhili wa *Nordic Development Fund (NDP).* Ni matarajio yetu kuwa mradi utatekelezwa mapema baada ya kuamua kufanya usanifu wa kina moja kwa moja ukifuatiwa na ujenzi wa kiwango cha lami.

(ii) Mheshimiwa Spika, Dodoma - Babati, usanifu wa kina wa barabara hii unatekelezwa na Kampuni ya *Carl Bro* ya Denmark. Kazi hizi zinagharamiwa kwa pamoja kati ya Serikali ya Tanzania, mkopo kutoka *Nordic Development Fund* na Benki ya Dunia. Kazi za usanifu wa kina zinatarajiwa kukamilika ifikapo mwezi Julai mwaka huu.

(iii) Mheshimiwa Spika, Babati - Minjingu, mradi huu ni sehemu ya barabara ya Singida - Babati hadi Minjingu unaogharamiwa kwa pamoja kati ya *Nordic Development Fund,* Benki ya Dunia na Serikali ya Tanzania. Usanifu wa barabara hii unatekelezwa na Kampuni ya *Carl Bro* ya Denmark vile vile na unatarajiwa kukamilika mwezi Julai, 2006.

(b) Mheshimiwa Spika, ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Iringa - Dodoma hadi Minjingu, utaanza mara baada ya kukamilika kwa usanifu wa kina ambao unatarajiwa kukamilika mwezi Oktoba, 2006 na kutegemeana pia na upatikanaji wa

fedha. Aidha, wakati wa kazi za usanifu zikiendelea, Serikali inaendelea kuwasiliana na wahisani mbalimbali ili kupata fedha za kugharamia ujenzi wa barabara hii.

**MHE. PASCHAL C. DEGERA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Aidha, namshukuru sana Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Lakini nina swali moja la nyongeza.

Pamoja na kwamba barabara hii ilitolewa ahadi katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi na aidha, Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete alipokuwa anafanya kampeni katika Mkoa wa Dodoma na hususan katika Wilaya ya Kondoa aliahidi kwamba barabara hii itajengwa kwa kiwango cha lami katika awamu ya kwanza ya utawala wake. Je, Wizara ina taarifa hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Spika, barabara hiyo aliyoitaja iko kwenye Ilani ya Uchaguzi kama alivyosema na vile vile Wizara ina taarifa na ahadi hiyo ya Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo nimeeleza kwenye jibu la msingi, ni nia ya Serikali kuhakikisha kwamba barabara hii ya kutoka Iringa - Dodoma kwenda Babati, inajengwa kwa kiwango cha lami na ndio maana tumesema kabla ya mwisho wa mwaka huu tutakuwa tumemaliza kazi ya upembuzi yakinifu pamoja na kufanya *detail design.* Kwa sasa Serikali inawasiliana na wafadhili mbalimbali kwa ajili ya kuhakikisha kwamba barabara hii inajengwa kwa kiwango cha lami. Kati ya wafadhili ambao Serikali inazungumza nao ni pamoja na *Nordic Development Fund, World Bank* pamoja na *ADB* na kwa kweli mawasiliano na *ADB* yameendelea hata mwaka huu, mwezi Januari 2006 tumeendelea kuwasiliana na *ADB* kwa ajili ya mkopo wa kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami. *(Makofi)*

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la dogo nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Miundombinu, nina swali la nyongeza.

Kwa kuwa sasa ni muda mrefu tangu tumeanza kuiomba Serikali kujenga barabara hii ya Minjingu - Dodoma - Iringa kwa kiwango cha lami na kwa kuwa barabara hii ni muhimu sana kwa maendeleo na uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, sasa Mheshimiwa Naibu Waziri anaweza kulielezea Bunge hili, upembuzi yakinifu unaweza kuchukua miaka mitano, sita mpaka 10. Maana ni muda mrefu sasa?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Spika, kwenye jibu la msingi nimeweka tarehe ambazo kazi za usanifu wa kina utakamilika na nimesema kwa kipande cha barabara ya kutoka Singida kwenda Minjingu na Dodoma kupitia Babati utakamilika mwishoni mwa mwezi

Julai, 2006 . Ile barabara ya Iringa kuja Dodoma hadi Babati itakamilika kufikia Oktoba, 2006 . Kwa hiyo, nimeeleza ni mwaka huu kazi hiyo ya usanifu itakamilika.

**MHE. MARIAM S. MFAKI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa katika jibu lake la msingi, Mheshimiwa Naibu Waziri kasema kwamba bado wanaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara hiyo kwa kiwango cha lami na kwa kuwa haijulikani mpaka sasa fedha hizo zitapatikana lini.

Mheshimiwa Spika, je, Naibu Waziri yuko tayari kuwaarifu wananchi wa Wilaya ya Kondoa kuhusu suala la ujenzi wa daraja ambalo ni kero kwa watumiaji ambalo liko eneo la Kolo, ni lini watakuwa tayari kulijenga?

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri na ya kueleweka ya Mheshimiwa Naibu Waziri wangu, lakini naona Waheshimiwa Wabunge wanazidi kusimama, simama. Naelewa kwamba wana shauku kubwa kwa sababu jambo hili limechukua muda mrefu.

Ningependa kuwahakikishia kwamba kwenye meza yangu jambo hili liko kwenye umuhimu wa kwanza, kwenye meza yangu mimi jambo hili liko kwenye umuhimu wa kwanza na mwisho baada ya Bunge hapa na kwenda ng'ambo kutafuta wafadhili ambao kimsingi watakuwa tayari kugharimia barabara hii na Waziri Mkuu anajua juu ya safari hiyo.

Pia ningependa vile vile Mheshimiwa Mbunge na wenzake waelewe kwamba wiki mbili zilizopita katika Wizara ya Fedha tumefanya kikao kikubwa pale cha mfadhili mwingine aliyejitokeza na barabara zilizotoka kwenye Wizara ya Miundombinu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hii ni moja wapo tunayoiombea fedha na mfadhili huyu nataka kumfuatilia kwa karibu. Kwa hiyo, ningependa lakini pamoja na hayo yote, fedha tunazoomba leo ni za makisio na tunajua kwamba kuna daraja, lakini unajua mambo haya hatutaki kufanya biashara ya rejareja hapa, sisi tunataka kufanya biashara kamili, daraja na barabara. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tunaendelea kumwomba Mwenyezi Mungu daraja hili lisianguke kabla ya mradi kuanza utekelezaji ili tuchanganye daraja na barabara kwenye mradi mmoja mzuri. Kwa hiyo, ningeomba waamini kwamba sisi tunaelewa habari za daraja. Tunaendelea kusali na tunatafuta fedha tunaendelea kusali na nafikiri Mungu atasikiliza kilio chetu. *(Makofi)*

Na. 102

**Uboreshaji wa Barabara za Kyela, Rungwe, Ileje, Mbozi, Mbinga na Rukwa**

**MHE. DR. HARRISON G. MWAKYEMBE** aliuliza:-

Kwa kuwa moja ya malengo makuu ya Serikali ya Awamu ya Nne ni kukuza kilimo kufikia asilimia 20; na kwa kuwa baadhi ya maeneo nchini yenye uwezo mkubwa wa kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara katika kipindi kifupi kama vile Kyela, Rungwe, Mbozi, Mbinga, Rukwa na kadhalika; kwa miaka mingi yanakwamishwa na tatizo la miundombinu mibovu hasa barabara.

Je, Serikali inakabiliana vipi na suala la uboreshaji wa barabara muhimu katika maeneo yaliyotajwa na mengine kama hayo katika muda mfupi ujao ili azma kuu ya Serikali ya kukuza kilimo kufikia asilimia 20 katika miaka mitano ijayo itimie?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe, Mbunge wa Kyela, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa yapo baadhi ya maeneo nchini yenye uwezo mkubwa wa kuzalisha mazao ya chakula na biashara lakini hayana barabara za uhakika.

Aidha, ili kukabiliana na suala la kuboresha barabara katika maeneo yaliyotajwa na mengineyo nchini, Serikali kupitia Wizara yangu imeandaa Mpango wa miaka kumi wa Maendeleo ya Barabara Nchini *(Ten Year Road Sector Development Programme)* 2001/2002 hadi 2010/2011. Utekelezaji wa mpango huu unaendelea na awamu ya kwanza ya miaka mitano itakamilika katika mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa mapitio yanafanyika katika mpango huo wa maendeleo ya barabara nchini ili kuhusisha barabara muhimu katika mpango huo ambazo au zilisahaulika au umuhimu wake umepanda zaidi katika kujenga uchumi wa Taifa.

Mheshimiwa Spika, pia Wizara ya Tawala za Mikoa ana Serikali za Mitaa inaandaa mpango kama huo kwa barabara za Wilaya na Miji ili nazo ziweze kuboreshwa. *(Makofi)*

**MHE. DR. HARRISON G. MWAKYEMBE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Nimefurahi kusikia kuhusu mpango wa miaka kumi wa Wizara. Nataka tu kuuliza kwamba kwa kufuata utaratibu ambao Mheshimiwa Rais ameuanza sasa hivi wa kuzifuata kero pale pale zilipo na kuzishambulia hapo hapo.

Je, Mheshimiwa Waziri anaweza akaja kuikagua barabara moja muhimu kweli kweli kiuzalishaji ya Kyela - Ipinda - Matema ambayo kila mwaka tangu Uhuru inageuka kuwa bwawa hivyo kuitenga kabisa Tarafa yenye utajiri mkubwa kwa kilimo ya Ntebelea

kwa miezi kadhaa na ambayo Mheshimiwa Rais alishawaahidi wana Kyela kwamba Serikali itaihangaikia? *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Spika, Mawaziri wa Serikali ya Awamu ya Nne kama ambavyo tumeahidi, tutafuata nyayo za Mheshimiwa Rais katika kushambulia matatizo ya wananchi huko huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana Waziri wangu toka juzi ameanza kushambulia barabara ya Dodoma - Manyoni hadi Singida na amerudi asubuhi hii. Mimi pia baada ya Bunge tu nitaanza kushambulia barabara ya Kibiti - Lindi na baadaye katika utaratibu huo nitafika kwenye barabara aliyotaja Mheshimiwa. *(Makofi)*

**MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali imeshaanza ujenzi wa barabara ya kando kando ya Ziwa Nyasa kuanzia Lituhi, Mbaha, Ngumbo, Liuli, *Mbamba bay,* Chiwanda hadi Chiwindi mpakani mwa Msumbiji lakini kwa kasi ndogo.

(i) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwahimiza makandarasi waliopewa barabara hizo ili kuhimiza uharaka wa kasi ili mazao yaweze kusafirishwa kwa haraka na wepesi?

(ii) Je, Serikali inaweza kuamuru makandarasi hao kuweka zaidi kokoto na changarawe badala ya udongo tifutifu na matope? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Miundombinu, jibu kwa sababu swali liliuliza na maeneo kama hayo. Kwa hiyo, hata Mbinga nako. *(Kicheko/Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Spika, kwa kweli Wizara yangu imepania kuhakikisha kwamba makandarasi wanaofanya kazi kwenye barabara zetu wanakwenda kwa *speed* kali na vile vile kwa kiwango kinachohitajika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunafuatilia kila wakati tunapopata taarifa kwamba mkandarasi fulani analegalega na kwa sababu Mheshimiwa Mbunge ametupatia taarifa hiyo tutaifuatilia mara moja. *(Makofi)*

Na. 103

**Mradi wa Kuvuta Maji kutoka Mto Wembere**

**MHE. DIANA M. CHILOLO** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali iliahidi kuvuta maji kutoka Mto Wembere hadi Mji Mdogo wa Shelui kwa lengo la kuwaondolea wananchi adha ya maji:-

Je, Serikali itaanza lini kutekeleza mradi huo?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Diana Chilolo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mradi wa maji wa Wembere - Shelui ulianzishwa na Serikali kwa madhumuni ya kuhudumia vijiji vitano vya Wembere, Nselembwe, Mgongo, Mseko na Kizonzo.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Mheshimiwa Mbunge ana haki ya kuufuatilia kwani ilipofika mwaka 1992, mradi huo ulifanikiwa kufikisha maji katika Mji wa Shelui na ulitoa huduma kwa muda wa miaka miwili tu na kuharibika. Uharibifu huo ulitokana na wizi wa mabomba ya chuma kwenye chanzo cha maji, kupasuliwa kwa mabomba na wafugaji kwa ajili ya kunyweshea mifugo, ukataji wa miti na kuchunga mifugo karibu na chanzo cha maji. Baadaye mabomba yalisombwa na maji katika Mto Shoka na Kironda kutokana na mvua kubwa zilizonyesha na kusababisha mafuriko.

Mheshimiwa Spika, juhudi za kufufua mradi huo zilianza mwaka 1996 kwa ushirikiano wa Halmashauri ya Wilaya na wahisani wa *Tanzania Christian Refugee Service (TCRS).* Mwaka 1998 mradi wa Shelui ulianza tena na ukafanya kazi kwa mwaka mmoja tu mpaka mwaka 1999. Mradi huo ulisimama tena kwa sababu ya kuibiwa mabomba na maji yalipungua kwenye chanzo cha maji.

Mheshimiwa Spika, Mji Mdogo wa Shelui upo katika mradi wa Majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijini, ambao sasa hivi unatekelezwa katika Wilaya ya Iramba kwa mkopo kutoka Benki ya Dunia. Katika mradi huo, wananchi wenyewe waliamua kuwa wachimbiwe visima badala ya kuvuta maji kutoka Mto Wembere. Hivyo, visima vitatu vimechimbwa chini ya mradi huo. Aidha, ujenzi wa miundombinu ya usambazaji wa maji yaani mabomba na matanki utaanza hivi karibuni kwa kuwa Kampuni ya kufanya kazi hiyo *(Tan Plant)* imekwishateuliwa na Halmashauri ya Wilaya.

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, naomba kuuliza swali la nyongeza linalofanana na hilo hilo hasa katika Kata za Ndago, Kinampanda na Urugu ambapo miradi hii ya Benki ya Dunia ipo kule. Wananchi walishachangia pesa kwa muda mrefu, lakini mradi huu mpaka sasa haujaanza. Ni lini sasa mradi huo utaanza ili kuwaondolea adha wananchi wa maeneo hayo? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kwa ufadhili wa Benki ya Dunia kuna miradi 15 ambayo inafadhiliwa katika Wilaya ya Iramba. Katika miradi hiyo 15 inayofadhiliwa mmojawapo ni mradi huo wa Ndago.

Kama nilivyosema awali ni kwamba mkandarasi yupo na wanaanza kazi, baada ya muda mradi wa Ndago na wenyewe utakuwa katika kutekelezwa. *(Makofi)*

**MHE. LAZARO S. NYALANDU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza.

Kwa kuwa katika miaka mitano iliyopita, miradi hii ya Benki ya Dunia ilikuwepo nchi nzima, Singida na mikoa mingine yote na kwa sababu kila mwaka utaratibu ulikuwa ni kuidhinisha vijiji vitano katika kila Halmashauri ya Wilaya ili hivi vijiji vichange kiasi fulani cha fedha katika mifuko ya fedha ya vijiji halafu na Halmashauri wa-*match* kile kiwango cha fedha na Benki ya Dunia watoe asilimia tisini.

Mheshimiwa Spika, vijiji vingi katika miaka mitano vilifanya hiyo kazi, lakini katika miaka mitano Singida kwa mfano, vijiji vitano tu ndiyo mpaka sasa hivi miradi yao bado haijakamilika. Je, Waziri yuko tayari kutoa tamko kwamba miradi ya Benki ya Dunia iruhusiwe kwa vijiji vyote Tanzania nzima na ni lini Benki ya Dunia itatoa fedha kwa ajili ya miradi hii kufanyika katika kila kijiji katika nchi hii maana mkopo uliopo naamini ni wa zaidi ya bilioni 300? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba miradi hii ya Benki ya Dunia ipo na kama nilivyosema kwenye jibu la nyongeza la mwanzo ni kwamba kwa Wilaya ya Iramba iko miradi 15 na kwa Wilaya ya Singida pia ipo miradi zaidi ya 15. Pia ni kweli kwamba wananchi wanatakiwa wachangie *5 percent* na Halmashauri *5 percent* na *90 percent* inatoa *World Bank* yenyewe. Lakini hata hivyo ni kwamba ili mradi utekelezwe ni lazima Halmashauri yenyewe ifanye uchaguzi ielekeze maeneo wanayoyaona na baada ya hapo usanifu ufanywe na pia maji yaangaliwe kama yapo ndipo mradi unapasishwa kuweza kuwa katika miradi ya Benki ya Dunia. *(Makofi)*

**SPIKA:** Naona Mheshimiwa Kabuzi Rwilomba, umesimama sana, umehangaika. Kwa hiyo, uliza swali la mwisho la nyongeza. *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kuniona. Nilifikiri labda hufahamu jina langu, kumbe unafahamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, matatizo yaliyoko katika maeneo ya Shelui na maeneo ya Iramba yanafanana sana na matatizo yaliyopo maeneo ya Geita na hasa Jimbo la Busanda ingawa liko karibu sana na Ziwa Victoria. Kuna mradi ambao ulianza mwaka 1976 wa kupeleka maji maeneo ya Katoro, Nyakagomba, Chigunga mpaka Busanda, lakini mradi huo umekuwa ukipewa fedha kidogo na hauishi kuanzia mwaka 1976. Kwa kuwa kuna miradi hii ya Benki ya Dunia ambayo Geita tunaiona ni kama ndoto na kwa kuwa mwaka huu umeingia kwa kasi mpya, je, mradi huu unaweza ukafikiriwa na wenyewe ukaisha? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAJI**: Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba miradi hii ya Benki ya Dunia kama nilivyosema ni Halmashauri yenyewe inateua. Lakini kwa mradi huo alioutaja wa mwaka 1976, miradi mingi ilikufa kwa sababu ya ushirikishwaji mdogo

wa wananchi na kwa hivi sasa kwa kuwa Wizara yangu inajitahidi na inaelekezana na Wilaya zote, wananchi wenyewe washirikishwe ili wamiliki hii miradi. Nina uhakika kwamba mradi huo ulioanza mwaka 1976 ukifufuliwa tena na ukipewa umiliki wa wanakijiji wenyewe hautakufa tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda nimshauri Mheshimiwa Mbunge kwamba akawasiliane na Halmashauri yake ili kuuweka mradi huo katika miradi ya Benki ya Dunia na pia ifanyiwe upembuzi yakinifu ili uonekane kama unafaa. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Swali la mwisho Mheshimiwa Dr. Zainab Gama. Ooh samahani, Mheshimiwa Waziri wa Maji ana majibu ya nyongeza.

**MBUNGE FULANI:** Waziri wa Maliasili na Utalii.

**SPIKA:** Aah, Utalii, Utalii. *(Kicheko)*

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII**: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Shemsa Mwangunga, Naibu Waziri wa Maji, napenda niongezee kuhusu mradi huo wa Nyakagomba kwamba mradi huo tumekuwa tukiupelekea fedha kwa kipindi cha miaka miwili, lakini usimamizi uliokuwa unafanywa na Halmashauri ya Wilaya ya Geita ulikuwa mbovu sana kiasi kwamba kila tunapopeleka fedha, fedha nyingi zinapotea.

Tumekuwa tukiwaambia na kuwashauri kwamba Halmashauri wawe na usimamizi mzuri zaidi kwa vile hata fedha za Benki ya Dunia au za Serikali zikipelekwa na zisiposimamiwa vizuri tatizo hilo litaendelea na mradi huo utabaki bila kumalizika. Kwa hiyo, naomba sana Mheshimiwa Mbunge atafute ufumbuzi wa tatizo hilo na itatusaidia sana kama Serikali. *(Makofi)*

Na. 104

**Ajira kwa Vijana**

**MHE . DR. ZAINAB A. GAMA** aliuliza: -

Kwa kuwa kumekuwepo na tatizo la ajira nchini hali inayosababisha vijana wengi hasa wale wenye kiwango kidogo cha elimu kushindwa kujiajiri wenyewe, kama vile wamachinga, mama lishe, wauzaji wa magazeti, wasukuma mikokoteni, wapiga debe kwenye vituo vya mabasi, wanamichezo, wasanii wa vijijini na mafundi wadogo wadogo:-

Je, Serikali ina mikakati gani ya kuwasaidia vijana hao katika kuendeleza ajira au shughuli zao ili waweze kushindana kibiashara katika soko la ushindani lisilojali ukubwa au udogo wa biashara ya mtu bali ubora wa bidhaa?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA (MHE. JEREMIAH S. SUMARI)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Zainab Gama, Mbunge wa Kibaha Mjini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Dr. Zainab Gama, kuwa ipo idadi kubwa sana ya vijana nchini ambao hawana ajira. Idadi hii ya vijana wasio na ajira inaongezeka mwaka hadi mwaka kutokana na vijana wengi wanaohitimu katika Elimu ya Msingi, Sekondari, Ufundi na Stadi za Kazi pamoja na Elimu ya Juu. Aidha, wako vijana ambao wamejiajiri katika sekta mbalimbali za uzalishaji ambao wanahitaji uwezeshaji na kuwekewa mazingira mazuri ya kazi ili waongeze uzalishaji, ubora wa bidhaa na tija. Vijana hawa ni pamoja na mafundi wadogo wadogo, wasukuma mikokoteni, mama lishe na wengine kama walivyoainishwa na Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imefanya zoezi kubwa la kuwatambua vijana wote waliojiajiri wenyewe katika Wilaya 76 hapa nchini ikiwemo na Wilaya ya Kibaha. Katika utafiti huo, Wizara imebaini aina 22 za vikundi vya vijana wanaojiajiri wenyewe katika Wilaya ya Kibaha. Aidha, Wizara pia imevifikia vijiwe vya vijana wengi ambao hawana ajira katika Wilaya ya Kibaha. Changamoto tuliyonayo ni kuwawezesha vijana waliojiajiri katika sekta ya uzalishaji mali kukabiliana na matatizo waliyonayo na kuwawezesha wengi wasio na ajira waajiriwe au wajiajiri wenyewe.

Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na changamoto iliyo mbele yetu, Wizara yangu inaandaa mikutano ya wadau ili kujadili tatizo la ukosefu wa ajira, matatizo ya wazalishaji wadogo wadogo na jinsi ya kupata mitaji kwa uzalishaji na biashara ndogo ndogo. Mikutano ya wadau itajumuisha vijana, *NGOs,* vyama vya vijana, vikundi vya vijana vya uzalishaji, washirika wa Kimataifa *(donors),* mashirika ya kijamii na ya kidini, wawakilishi wa Wizara na sekta muafaka kwa ajira za vijana na wataalam wawezeshaji. Mikutano hii ya wadau itafanyika katika kila mkoa ikiwa ni pamoja na mkoa wa Pwani.

Mheshimiwa Spika, tunaamini kuwa matatizo mengi na yanayowakabili vijana wetu yataibuliwa katika mikutano ya wadau. Aidha, njia ya kupata majawabu ya baadhi ya matatizo pia itajitokeza. Wizara itatumia matokeo haya kuandaa mpango wa kutatua matatizo na kuondoa vikwazo vinavyowakabili vijana kwa ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya. Hata hivyo, matatizo ya upatikanaji wa mitaji kwa ajili ya kuanzisha na kuendeleza biashara na uzalishaji mdogo mdogo yatajitokeza. Wizara yangu imepanga kushirikiana na Waheshimiwa Wabunge kulitafutia ufumbuzi suala hili mapema iwezekanavyo. *(Makofi)*

Moja ya njia ya kuwawezesha vijana kupata mitaji kwa ajili ya uzalishaji mali na kujiajiri ni mikopo kutoka kwenye Vyama vya Ushirika wa Kuweka na Kukopa. Ili kuanza haraka, Wizara yangu inafanya marekebisho katika Mfuko wa Maendeleo ya Vijana ili uweze kuwasaidia vijana kuwa na fedha za kianzio cha kukopeshana wanapoanzisha *SACCOS* zao. Aidha, Wizara yangu inaandaa pendekezo kwa Serikali kuongeza mtaji wa mfuko huu. Katika kufanikisha uanzishaji wa vyama hivi haraka,

Wizara yangu inaomba ushirikiano wa Wakuu wa Mikoa, Waheshimiwa Wabunge, Wakuu wa Wilaya na Halmashauri za Wilaya ili kuanzisha angalau *SACCOS* moja ya vijana katika kila tarafa hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mifuko inayosaidia washirika kama *SCULT* na *SELF,* wafadhili na baadhi ya mabenki yako tayari kusaidiana na Serikali katika vita hii, upatikanaji wa mitaji ili kupanua suala la ajira. Lengo letu ni kuwawezesha vijana wasiopungua laki saba kupata mitaji ya kujiajiri wenyewe katika kilimo, ufugaji, uvuvi, uchimbaji madini mdogo mdogo, uzalishaji mali na kusindika mazao ya kilimo, utalii, ufundi na sanaa kupitia vyama vya *SACCOS.*

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi itapanua mafunzo ya ufundi na stadi za kazi ili wahitimu wa shule za msingi na sekondari wapate ujuzi wa kuwawezesha kujiajiri na kuajiriwa.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inampongeza sana Mheshimiwa Dr. Zainab Gama, kwa kazi kubwa anayoifanya kuwahamasisha vijana, akinamama na wananchi kwa ujumla katika shughuli za uzalishaji mali. Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge ushirikiano wa Wizara yangu katika kufanikisha kazi hii. *(Makofi)*

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri naomba kuuliza. Kwa kuwa mkombozi mkubwa wa makundi yote haya ni *SIDO,* je, Serikali itakubaliana nami kwamba sasa ni wakati muafaka wa kuendeleza *SIDO* mijini na vijijini?

**WAZIRI WA VIWANDA , BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, kweli tumeangalia katika suala zima la kuwawezesha vijana *SIDO* ina nafasi kubwa Tanzania. Sasa hivi *SIDO* ina matawi mengi, lakini yako mikoani. Katika Bajeti yetu ijayo tutaangalia jinsi gani ya kuweza kufikisha *SIDO* hata Wilayani ili iwe mkombozi wa vijana. *(Makofi)*

**MHE. WILLIAM J. KUSILA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Kwa kuwa ipo sheria ya nguvu kazi ambayo kimsingi inamtaka kila mtu mwenye uwezo wa kufanya kazi afanye na kwa kuwa kwa muda mrefu tutaendelea kutegemea kilimo kuwa ndiyo mwajiri mama katika nchi hii na kwa kuwa vijana wengi vijijini hawataki kujishirikisha na kilimo, je, Serikali ina mpango au ina kusudio lolote la kuitumia sheria hii ya nguvu kazi kuhakikisha kwamba vijana walio vijijini wanajishirikisha na kilimo na kuwasaidia ili kilimo chao kiwe cha tija?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA (MHE. JEREMIAH S. SUMARI):** Mheshimiwa Spika, Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana itatumia sheria zote zilizopo ikiwa ni pamoja na ya nguvukazi kuwahimiza vijana wetu kufanya kazi na kuendelea kuwashauri umuhimu wa kufanya kazi. *(Makofi)*

**MHE. AMINA C. MPAKANJIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali moja dogo la nyongeza kama ifuatavyo: -

Nadhani wengi tunafahamu moja kati ya *agenda* kubwa kabisa za Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wa Awamu hii ya Nne ilikuwa ni ajira kwa vijana na yeye mwenyewe alisema kwamba amegundua kwamba tatizo hili ni kubwa na kweli vijana wanahitaji ajira na aliahidi na vijana wana matarajio kwamba kweli kwa sasa hivi katika awamu hii ya nne watapata ajira nyingi sana, lakini pia vile vile nadhani...

**MBUNGE FULANI:** Swali.

**MHE. AMINA C. MPAKANJIA:** Nauliza ndiyo swali lenyewe. Lakini pia vile vile nadhani Mheshimiwa Naibu Waziri atakubaliana nami kwamba vijana wengi hawana mafunzo ya uzalishaji mali. Je, Serikali ya Awamu ya Nne kwa kushirikiana na Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana ina mpango gani wa kuanzisha vituo vya mafunzo vya uzalishaji mali kwa vijana ili hata kama kweli watakuja kupewa hiyo mikopo, hata kama kweli watakuja kupewa mitaji waweze kuitumia ipasavyo kuliko kuja kupewa ajira, lakini kwa sababu vijana hawana mafunzo ya uzalishaji mali tukawa kama vile tunapoteza. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, swali refu, sijui jibu nalo litakuwa refu? *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA (MHE. JEREMIAH S. SUMARI):** Mheshimiwa Spika, ni kweli katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi umuhimu wa ajira kwa vijana upo. Asilimia 70 ya nguvukazi ya nchi yetu ni vijana, ndiyo sababu katika jibu la msingi tumesema kwamba kazi yetu Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana ni kutafuta ajira laki saba. Tayari tunavyo vituo vitatu chini ya Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana kwa ajili ya kuwaendeleza vijana. Kituo kimoja kiko kule Ilonga kule Kilosa, kingine kiko Mbozi Sasanda na cha tatu kiko kule Marangu. Vituo hivyo vitatu pamoja na vituo vya *VETA* vikishirikiana tunaamini kwamba tayari tunao mfumo wa kutuwezesha kuwafundisha na kuwashauri vijana wetu kwa ajili ya kujijengea ujasiriamali na uwezo wa kuzalisha bidhaa zinazoweza kumudu soko linalohitajika. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Spika, ningependa kumshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri na kuongezea kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imepanga kupanua mafunzo ya *VETA* na stadi za kazi kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, pamoja na mafunzo ya ujasiriamali kupitia Shirika la *SIDO.* Hivyo, tunategemea kwamba vijana wote ambao watafaidika na mikopo aliyoiainisha Mheshimiwa Naibu Waziri watapewa mafunzo hayo kabla ya kupata mikopo hiyo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali yamekwisha. Kabla hatujaingia katika hatua inayofuata, nayo ni kutangaza matokeo ya kazi yetu ya jana ninayo matangazo machache yafuatayo, kwanza ni Kamati. Kamati ya Mambo ya Nje mnaombwa kukutana saa 5.00 chumba namba 231 jengo la utawala ghorofa ya pili. Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, Waheshimiwa mnaombwa kukutana mara baada ya kipindi hiki cha Maswali na Majibu chumba namba 219 ghorofa ya pili.

Wabunge walio wanachama wa Chama cha Wabunge dhidi ya UKIMWI *(TAPAC)* pamoja na wengine wote Wabunge ambao wangependa kusikia shughuli za *TAPAC* mnaombwa kubaki ndani ya ukumbi baada ya shughuli zetu kwisha kwa asubuhi hii. Tangazo lingine ni kwamba kutakuwa na hafla ya uzinduzi wa *Agape Television Network (ATN)* Dodoma na hafla hiyo itafanyika *Dodoma Hotel* saa 2.00 usiku leo jioni.

Waheshimiwa Wabunge, tangazo la mwisho kwa haya niliyonayo ni kwamba kama nilivyotangaza awali kutakuwa na semina ya siku tatu kuanzia Jumatatu ambayo inaitwa *Post Election Seminar.* Hii ni kuchangia uzoefu kuhusu masuala mbalimbali ya chaguzi katika Bara letu la Afrika. Siyo *Post Election Seminar* kwa maana tu ya kutathmini yetu ya hapa, lakini pia ni kutazama na yaliyotokea katika nchi nyingine zenye mazingira ambayo tunafanana. *(Makofi)*

Semina hii ni nzito na baadhi ya wazungumzaji tunaowatarajia na wameishathibitisha kuja ni Mheshimiwa Francis Ole Kaparo, Spika wa Bunge la Kenya, Mheshimiwa Alban Bargbin; Kiongozi wa Upinzani wa Bunge la Ghana, Mheshimiwa Denis Marshal, Katibu Mkuu wa *Commonwealth Parliamentary Association* na Mheshimiwa Debora Della, mtaalam kutoka Bunge la Canada. Hawa ni baadhi tu ya *resource persons* tutakaokuwa nao kwa semina hii muhimu sana na kwa sababu ndiyo tumetoka kwenye uchaguzi nawasihi Waheshimiwa Wabunge wote tubaki, tutahudumiwa ili tuhudhurie semina hii. *(Makofi)*

Baada ya hayo sasa namwomba Katibu wa Bunge kama *returning officer* wetu aweze kutangaza matokeo ya uchaguzi wa jana.

## MATOKEO YA UCHAGUZI

**ND. DAMIAN S. L. FOKA - KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, jana tulifanya chaguzi mbalimbali za Wabunge wa kuwakilisha Bunge hili katika vyombo mbalimbali vya Kibunge. Tulianza na uchaguzi wa Wajumbe wawakilishi wa *ACP-EU.* Wagombea walikuwa ni wawili.

Kwanza ni Mheshimiwa Balozi Abdi Mshangama, wa pili ni Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi. Kura zilizopigwa ni 260, kura zilizoharibika ni mbili na kura halali ni 258. Matokeo ni kwamba, Mheshimiwa Balozi Abdi Mshangama alipata kura 76 na Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi amepata kura 182.

Bunge linahitaji mwakilishi mmoja kwa hiyo, namtangaza Mheshimiwa Kilontsi M. Mporogomyi, kuwa ndiyo mwakilishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, matokeo ya uchaguzi wa wawakilishi katika Bodi za Vyuo. Wagombea walikuwa watano wengine walijitoa. Waheshimiwa Wabunge ambao walijitoa ni Mheshimiwa Ruth Msafiri na Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji kwa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Kwa sababu walikuwa wamejitoa na waliobaki wakawa ni watatu na wanaohitajika ni watatu, kwa hiyo, naomba kuwatamka wafuatao kuwa ndiyo wawakilishi wa Bunge hili katika Baraza la Chuo Kikuu Dar es Salaam. Mheshimiwa Profesa Raphael Mwalyosi, Mheshimiwa Profesa Feethan Filipo Banyikwa na Mheshimiwa Susana Lyimo kutoka Upinzani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Chuo Kikuu cha Kilimo (*SUA*). Waliopiga kura ni 266, kura zilizoharibika ni moja. Kwa hiyo, kura halisi ni 265. Naomba kutangaza matokeo kama ifuatavyo. Mheshimiwa Castor Ligallama alipata kura 28; Mheshimiwa Gaudence Kayombo amepata kura 247; Mheshimiwa Dr. Mzeru Nibuka kura 250. Wanahitajika wawakilishi watatu. Naomba kuwatangaza washindi kuwa ni Mheshimiwa Dr. Mzeru Nibuka; Mheshimiwa Gaudence Kayombo na Mheshimiwa Chacha Wangwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uchaguzi wa Chuo Kikuu Huria. Waliopiga kura ni 267, kura zilizoharibika 3, kura halali 264. Matokeo ya uchaguzi ilikuwa ni kama ifuatavyo. Mheshimiwa Benson Mpesya kura 203, Mheshimiwa Beatrice Shellukindo kura 217. Kwa kuwa wanaohitajika ni watatu wafuatao ndiyo watakuwa wawakilishi. Mheshimiwa Beatrice Shellukindo kura 217; Mheshimiwa Benson Mpesya kura 208 na Dr. Ali Tarab Ali huyu alipita bila kupingwa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hebu mwenye neno la kusema asimame ili Spika amwone. Naona kama kuna kama manung'uniko hivi.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Spika, walikuwa wagombea watatu kwa Chama cha Mapinduzi lakini unaotutajia ni wawili tu.

**SPIKA:** Katibu ilibidi kutaja watatu pamoja na huyu mwingine atakuwa alipita bila kupingwa na kura zake.

**ND. DAMIAN S. L. FOKA - KATIBU WA BUNGE:** Ni Mheshimiwa Juma Njwayo ambaye kwa bahati mbaya kura nilizoletewa hapa nafikiri zitakuwa ni mwakilishi mwingine lakini naomba nitalisahihisha hilo baadaye.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, waliopita ni wawili kwa CCM na mmoja Vyama vya Upinzani. Tulizozikosa wamechanganya kura baina ya *SUA* nadhani na chuo kingine za yule wa tatu. Kwa hiyo, tutazijua lakini hazisaidii kubadili chochote. *(Makofi)*

**ND. DAMIAN S. L. FOKA - KATIBU WA BUNGE:** Matokeo ya Chuo Kikuu cha Mzumbe ambapo tuna mwakilishi mmoja naye huyu alipita bila kupingwa ni Mheshimiwa Dr. Godfrey Zambi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaingia kundi la *SADC* . Kundi la wanaume waliopigiwa kura ni hawa wafuatao. Mheshimiwa Richard S. Nyaulawa na Mheshimiwa Mbaruk Kassim Mwandoro. Kura zilizopigwa ni 267, zilizohabirika ni 6 kura halali ni 261. Matokeo, yake ni kama ifuatavyo. Mheshimiwa Mbaruk Kasim Mwandoro amepata kura 114, Mheshimiwa Richard S. Nyaulawa amepata kura 147. Hapa namtangaza Mheshimiwa Richard S. Nyaulawa kuwa mshindi. *(Makofi)*

Kundi la wanawake, waliogombea hapa ni hawa wafuatao. Mheshimiwa Halima Mamuya alijiondoa; Mheshimiwa Ruth Msafiri; Mheshimiwa Dr. Lucy Nkya; Mheshimiwa *Engineer* Stella Manyanya. Matokeo yao ni kama ifuatavyo. Mheshimiwa Ruth Msafiri amepata kura 67; Mheshimiwa Dr. Lucy Nkya amepata kura 83; Mheshimiwa *Engineer* Stella Manyanya kura 114. Wanaotakiwa ni watatu kwa hiyo, nawatangaza wawakilishi kama ifuatavyo. Ni Mheshimiwa *Engineer* Stella Manyanya, Mheshimiwa Richard S. Nyaulawa na Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, ambaye alipita bila kupingwa. *(Makofi)*

**MHE. DR. MILTON M. MAHANGA:** Mheshimiwa Spika, kwa sababu *SADC* tunawakilishwa na wawakilishi na wajumbe wanne tungetajiwa jina la mwana mama huyo maana wengine hatumjui, hata Mwenyekiti wa Bunge wa akina mama ambaye naye anaungana nao tutajiwe ili tumfahamu. *(Makofi)*

**ND. DAMIAN S. L. FOKA - KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, bado nilikuwa sijaletewa jina, lakini nasikia mnong'ono ni Mheshimiwa Anne Makinda. *(Makofi)*

Sasa ni uchaguzi kwa Bunge la Afrika. Mlikuwa mnajaza nafasi mbili na waliojitokeza kutoka kundi la Zanzibar ni hawa wafuatao. Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji na Mheshimiwa Omar Sheha Mussa. Kura zilizopigwa ni 267 kura zilizoharibika ni 3 kura halali ni 264. Matokeo ni kama ifuatavyo. Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji amepata kura 102, Mheshimiwa Omar Sheha Mussa amepata kura 162. Kwa hiyo, namtangaza Mheshimiwa Omar Sheha Mussa kuwa ndiye mwakilishi kutoka upande Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kutoka kundi la Tanzania Bara kulikuwa na wagombea wawili ambao ni Mheshimiwa William Kusila na Mheshimiwa Dr. James Wanyancha. Kura zilizopigwa ni 267, zilizoharibika ni mbili kura halali ni 265. Matokeo ni kama ifuatavyo. Mheshimiwa William Kusila kura 59; Mheshimiwa Dr. James Wanyancha kura 206. Kwa matokeo haya wawakilishi wetu sasa wanaoungana na wale wengine ambao waliochaguliwa katika mkutano uliotangulia ni Mheshimiwa Omar Sheha Mussa na Mheshimiwa Dr. James Wanyancha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaingia uchaguzi wa Tume ya Huduma za Bunge. Kundi la wanawake kura zilizopigwa ni 267 hakuna iliyoharibika. Matokeo ni kama ifuatavyo. Mheshimiwa Dr. Zainab Gama kura 45; Mheshimiwa Kidawa Saleh kura 109; Mheshimiwa Estherina Kilasi kura 113. Anatakiwa mmoja kutoka kundi la wanawake na kwa ajili hiyo namtangaza Mheshimiwa Estherina Kilasi kama mwakilishi wa Tume ya Huduma za Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kundi la Kambi ya Upinzani, wakati wa kupiga kura kwa ajili ya kundi hili, waliopiga kura ni 267, kura zilizoharibika ni 3 kura halali ni 264. Matokeo ni kama ifuatavyo. Mheshimiwa Khalifa S. Khalifa kura 62; Mheshimiwa Philemon Ndesamburo amepata kura 202. Mwakilishi wa kundi hili ni Mheshimiwa Philemon Ndesamburo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kundi la jumla, kulikuwa na wagombea 11. Kura zilizopigwa ni 267 hakuna kura iliyoharibika. Matokeo ni kama ifuatavyo. Mheshimiwa Balozi Abdi Mshangama amepata kura 11; Mheshimiwa Magalle Shibuda amepata kura 18; Mheshimiwa Raynald Mrope amepata kura 29; Mheshimiwa Mohammed S. Soud amepata kura 49; Mheshimiwa Yahya Kassim Issa amepata kura 68; Mheshimiwa Aggrey D. J. Mwanri kura 75; Mheshimiwa Mgana Msindai kura 77; Mheshimiwa Lucas amepata kura 80; Mheshimiwa William Shellukindo amepata kura 128; Mheshimiwa Abdulkarim Shah amepata kura 133; Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya amepata kura 165. Kutoka kundi hili wanatakiwa wawakilishi watatu. Naomba kuwatangaza wafuatao kuwa ndiyo wawakilishi wa Bunge ambao ni Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya; Mheshimiwa Abdulkarim Shah na Mheshimiwa William Shellukindo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa Wabunge waliochaguliwa kwa ajili ya Bunge la Afrika Mashariki ni hawa wafuatao ambao walithibitishwa na Bunge hili jana. Mheshimiwa Dr. Norman Sigalla na Mheshimiwa Hulda Kibacha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hapa ni mwisho wa matokeo ya uchaguzi ambao Bunge lilifanya jana, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Kuna neno lolote kuhusu uchaguzi?

**WABUNGE FULANI:** Hapana!

**SPIKA:** Tumefunga, tumemaliza, ahsante sana Katibu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nilipotangaza mikutano ya Kamati walikuwa wameitana mara baada ya kipindi cha maswali lakini kama mnavyofahamu hivi punde tutamwita Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa sababu shughuli za Bunge naona zimekwisha na kama kawaida msemaji wetu wa mwisho anakuwa ni Waziri Mkuu kuhitimisha mkutano wetu. Kwa hiyo, ninashauri Waheshimiwa Wabunge wasitoke sasa kwenye Kamati badala yake tuweze kubaki kusikiliza hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu wetu.

Wakati huo naomba hawa wanachama wa *Amani Forum* nao watakutana, sasa wametaja chumba kile kile ambacho kina mkutano mwingine, nadhani watasikilizana huko baada ya kufika. *Amani Forum* chumba namba 231 baada ya kuahirisha Bunge. Sasa namwita Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

## KUAHIRISHA BUNGE

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, huu ni Mkutano wetu wa Pili wa Bunge lako Tukufu tangu tuchaguliwe kuwa wawakilishi wa wananchi. Katika mkutano huu ambao shughuli zake zinamalizika leo. Hati 10 ziliwasilishwa Mezani na Serikali ilijibu maswali 104 ya msingi na maswali mengine ya nyongeza yaliulizwa na Waheshimiwa Wabunge.

Aidha, Waheshimiwa Wabunge waliweza kujadili na kupitisha Azimio la Kuridhia Itifaki ya Kuanzishwa kwa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu pamoja na Azimio la Kuridhia Itifaki ya Kuanzishwa Mahakama ya Afrika. Kukubali kuridhia maazimio hayo ni kielelezo cha dhati kwamba Tanzania ni nchi inayothamini haki za binadamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Bunge hili pili liliweza kujadili kwa mapana hotuba ya Rais, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, aliyoitoa hapa Bungeni tarehe 30 Desemba 2005 na hatimaye Bunge lako lilipitisha Azimio la kushirikiana naye katika kutekeleza yote yaliyomo katika hotuba hiyo. Mjadala ulikuwa mzuri na wenye matumaini makubwa kwa wananchi. Wananchi wanategemea sana kwamba tutawaongoza katika kutekeleza yote yale yaliyoagizwa katika hotuba ya Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mkutano huu ulikuwa mkutano wetu wa kwanza wa kazi tangu uchaguzi mkuu ulipokamilika. Aidha mkutano huu umefanyika baada ya Waheshimiwa Wabunge wote kuhudhuria semina ili kufafanuliwa kanuni na taratibu za vikao vya Bunge na yale yanayostahili kufanyika wakati wa vikao ndani ya Bunge. Tumepata uzoefu wa kwanza wa matumizi ya Kanuni za Bunge, tukiwa ndani ya Bunge. Napenda kumshukuru Mheshimiwa Spika na Naibu Spika kwa kutuongoza vizuri kufuata Kanuni za Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge, wote tuliopata nafasi ya kutoa hotuba zetu humu ndani kwa mara ya kwanza tulianza hotuba zetu kwa kuwashukuru wananchi waliotuchagua na kutuwezesha kufika Bungeni. Hapakuwepo na hata mmoja wetu aliyesimama na kusema kwamba yuko ndani ya Bunge hili kwa makosa. Wote tumeingia Bungeni kwa kuchaguliwa katika uchaguzi uliokuwa huru na haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kurudia tena pongezi zangu kwa Tume ya Uchaguzi kwa kufanya kazi nzuri sana katika uchaguzi uliopita. Kwa msingi huo, ni wajibu wetu kulinda uhuru na haki ya kidemokrasia ambayo imetuwezesha kuingia hapa Bungeni. Nawasihi tutumie fursa hii kipindi cha miaka mitano ijayo kuendelea kuimarisha utamaduni wa kushirikiana na kuhakikisha kuwa viongozi wa vyama vya siasa wanaandaa na kuzinadi sera zao kwa kuzingatia umuhimu wa kulinda Utaifa wetu. Tutumie uhuru tulionao kwa busara na kwa kiasi bila kuvuka mipaka. Huu ndiyo utamaduni wa Mtanzania tunayo kila sababu ya kuuendeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Bunge hili limejadili kwa kina kama nilivyosema hotuba ya Rais ambayo imetoa mwelekeo na majukumu ya msingi ya Serikali ya Awamu ya Nne. Kazi kubwa iliyo mbele yetu sasa inahitaji ushirikiano wa hali ya juu ili kuongeza kasi ya

maendeleo ya nchi yetu. Tukiwa legelege hatutatimiza malengo yetu ya kutuwezesha kuhimili ushindani wa kiuchumi ulioko hivi sasa. Lazima tuongeze juhudi zaidi na kama Marehemu Baba wa Taifa, Mwalimu J. K. Nyerere, alituasa kwamba lazima tukimbie wakati wenzetu walioendelea wanatembea. *(Makofi)*

Tushirikiane katika kutimiza malengo yetu ili kukuza uchumi wa nchi yetu. Kwa msingi huo, ni lazima tujipange vizuri, lazima tuelewane tangu awali kuwa wote hatuwezi kuwa watoa maagizo au watoa amri, lazima kila mmoja kwa nafasi yake aelewe wajibu wake na autekeleze. Kama ni Mkuu wa Mkoa au wa Wilaya au Mkurugenzi wa Halmashauri au Waheshimiwa Wabunge na Madiwani, ni lazima sasa kila mmoja aelewe anatakiwa kufanya nini, atatekelezaji haya anayoagizwa na atashirikiana vipi na wananchi ili kufikia malengo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, labda nifafanue kwa kugusia baadhi ya maeneo. Hivi sasa tunayo misingi imara ya kiuchumi na kisiasa. Nchi yetu inayo amani, tunao uongozi thabiti chini ya Rais Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete. *(Makofi)*

Mheshimiwa Rais ana malengo na dhamira ya dhati ya kuleta mabadiliko katika nyanja mbalimbali ili kuboresha maisha ya kila Mtanzania. Maendeleo yetu na mafanikio katika kukabiliana na changamoto zilizo mbele yetu yapo mikononi mwetu. Lazima tutumie uwezo wetu kikamilifu wa rasilimali watu, fedha na maliasili ili kutimiza dhamira ya Rais wetu. Swali ambalo sisi viongozi na watendaji Serikalini hatuna budi tujiulize ni je, tupo tayari kusaidiana na Mheshimiwa Rais, tunayo dhamira ya kuthubutu kutoa maamuzi na kutekeleza yale yote yanayotufikisha kwenye malengo yetu? Wito wangu ni kuwa hatuna namna ya kukwepa wajibu huu, tuliukubali na kwa hiyo, tusirudi nyuma. Lazima tuelewane kuwa kiongozi au mtendaji kutokufanya lolote kabisa kwa yale yanayomhusu ni kutowajibika. Lakini kufanya kila lililo ndani ya uwezo wetu ni wajibu wa kwanza kabisa wa kiongozi. Ni vema basi tuonyeshe dhamira hiyo kwa vitendo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo moja ambalo japo halihitaji fedha lakini linawakera sana wananchi na linaonyesha uwajibikaji hafifu wa viongozi na watendaji ni kutoshughulikiwa kwa kero za wananchi mbalimbali. Dhana ya utawala bora lazima ishuke hadi katika ngazi ya kijiji na mtaa. Swali ambalo najiuliza bila kupata majibu ya kuridhisha hivi ni kwa nini mwananchi asafiri kwa mfano kutoka Nkasi au Karagwe hadi Dar es Salaam au Dodoma kuja kumuona Waziri Mkuu au hata Mheshimiwa Rais kwa tatizo au kero ambayo inaweza kupatiwa ufumbuzi katika ngazi za chini? Afisa Mtendaji wa Kijiji au mtaa yupo, Katibu Tarafa yupo, Mkuu wa Wilaya yupo, Mkuu wa Mkoa yupo, tatizo ni nini? Je, ni uwezo hawana? Lazima tubadili hali, lazima kila mamlaka iwajibike na ibebe dhamana yake kikamilifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Waziri Mkuu, inapotekeleza kazi za Mkuu wa Mkoa au Mkuu wa Wilaya, ni wazi viongozi hao wameshindwa kufanyakazi zao na hawana sababu ya kuendelea kuwepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali iliyoko madarakani inayo muda maalum wa kutekeleza ahadi zake kwa wananchi. Katika muda huo, tumedhamiria kutekeleza malengo yetu kwa viwango vya juu kabisa. Lakini lazima sisi tulio ndani ya Serikali tuelewane. Kama sote tunaelewa tunakoelekea, tukafuata Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2005, tutafika.

Mheshimiwa Spika, vile vile zipo ahadi maalum za Mheshimiwa Rais alizozitoa wakati akiomba kura, zipo ahadi za sisi Waheshimiwa Wabunge, zipo pia ahadi za Waheshimiwa Madiwani. Jambo muhimu ambalo lazima tulidhamirie ni kupunguza pengo kati ya ahadi na utekelezaji wake. Katika kufanya hivyo lazima tujipange vizuri.

Mheshimiwa Spika, yapo majukumu ya Serikali za Mitaa na Mkoa lakini vile vile yapo majukumu ya Serikali Kuu. Serikali Kuu yenye uwezo wa mwisho wa Kiserikali kwa mujibu wa Katiba kwa kupitia viongozi, Taasisi na Mamlaka mbalimbali zinaweza kutoa maelekezo yanayozitaka Serikali za Mitaa kuzingatia Sheria, Kanuni na miongozo mbalimbali katika utendaji wao wa kazi au kuweka kipaumbele mahsusi kwa masuala yaliyoainishwa kwenye uharaka na umuhimu. Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya wanatakiwa kufuatilia na kuhakikisha kuwa maagizo na maelekezo hayo ya Serikali katika Halmashauri yanatekelezwa kama ilivyoelekezwa. Kwa sababu Serikali za Mitaa ziko karibu na wananchi. Tunapeleka fedha nyingi sana huku kwa ajili ya shughuli mbalimbali za maendeleo. Ni wajibu wa viongozi hawa wa Mikoa na Wilaya watambue hilo na kuhakikisha matumizi ya fedha hizo yanasimamiwa vizuri ili kukidhi matarajio ya wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivi sasa sote kama Taifa tunakabiliwa na changamoto kubwa ya kuhakikisha kwamba matatizo ya upungufu wa umeme, ukame mkubwa na uharibifu wa mazingira hayapunguzi kasi ya ukuaji wa uchumi wetu. Hiki ndicho kipindi cha viongozi katika ngazi mbalimbali nchini kuonyesha uwezo wao katika kumsaidia Mheshimiwa Rais kuongoza Taifa katika kukabiliana na matatizo haya. Ndani ya Serikali na vyombo vingine vya dola tunahitaji viongozi na watendaji wepesi lakini makini katika kutoa maamuzi yenye kuleta nafuu kwa wananchi ili waweze angalau kumudu kukabiliana na matatizo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili tufanikiwe, ni wajibu wetu kuhakikisha kuwa rasilimali kubwa tuliyonayo yaani rasilimali watu inatumika kikamilifu. Matokeo ya sensa ya mwaka 2002 yalionyesha kuwa idadi ya Watanzania walio kati ya umri wa miaka 18 hadi 60 ni asilimia 39.6 ya Watanzania wote.

Mheshimiwa Spika, hili ndilo kundi linalotegemewa kuleta mabadiliko nchini. Ni wajibu wetu kujipanga vizuri kila mtu kwa nafasi yake ili tuweze kutimiza malengo ya kuleta mabadiliko kwa wananchi. Hata hivyo, eneo moja ambalo bado naliona kuwa ni kikwazo katika matumizi ya rasilimali watu ni suala la matumizi ya muda. Muda ni rasilimali muhimu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali tunalopaswa kujiuliza ni je tunatumiaje muda katika maeneo yetu ya kazi. Kwa mfano, kila mfanyakazi ajiulize katika muda wa saa 8 anapokuwa katika eneo lake la kazi anafanya nini cha kuongeza tija?

Takwimu za matumizi ya muda zinaonyesha kuwa katika nchi zinazoendelea wastani wa matumizi ya muda wa kazi kikamilifu ni kati ya saa 13 hadi saa 26 kwa wiki, wakati katika nchi zilizoendelea wastani wao ni kati ya saa 40 hadi 70 kwa wiki.

Ni wazi basi kuwa tunapoteza muda wetu mwingi kwa siku kwa mambo yasiyo na tija. Ni lazima tuelewe kuwa hatuna muda wa kusubiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Watanzania wanahitaji mabadiliko, wanahitaji kuona ahadi zilizotolewa zikitekelezwa. Wanahitaji kuona vitendo vya watendaji wa Serikali na Taasisi za Umma zikifanana na zile za Rais Jakaya Mrisho Kikwete. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini napenda kutoa tahadhari ndani ya Bunge lako Tukufu kwamba kila Mtanzania ana nafasi na wajibu wake katika kujiletea maisha bora. Kwa maana hiyo, kila mmoja wetu lazima ahakikishe kuwa ule utaratibu wa kufanya kazi iwe za ofisini, mashambani au kwenye migodi kwa mazoea unapigwa vita. *It is not business as usual.* Hii ndiyo tafsiri ya ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tija katika sehemu za kazi itaongezeka kwa kasi zaidi endapo tutaendeleza matumizi ya sayansi, teknolojia na ubunifu katika utendaji kazi. Utendaji kazi usio na ubunifu kamwe hautuwezeshi kwenda kwa kasi tunayotaka na kukabiliana na utandawazi. Tafiti nyingi kuhusu masuala ya utandawazi na uchumi wa Kimataifa zinaonyesha kuwa sayansi, teknolojia na ubunifu ni misingi na kichocheo muhimu kilichowezesha nchi tajiri kupiga hatua za kimaendeleo.

Hata hivyo, kiwango cha matumizi ya sayansi, teknolojia na ubunifu katika nchi zinazoendelea ni kidogo. Hapa nchini tunajivunia na tunao wataalam wengi katika nafasi mbalimbali. Nina hakika wananchi wetu wangependa wataalam wetu waongeze ubunifu katika kutatua matatizo na kero za wananchi.

Mheshimiwa Spika, katika mazingira ya sasa watendaji wanaokaa ofisini na kusubiri hadi majalada yatoke kwa viongozi wao, wanasubiri kusimamiwa kila wakati ndipo wafanye kazi hawezi kuendelea na kasi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lazima tutumie sayansi, teknolojia na ubunifu katika mabadiliko ya haraka ya kiuchumi na ya kijamii. Changamoto kubwa ndani ya Serikali ni jinsi ya kuhakikisha kuwa matumizi ya sayansi, teknolojia, ubunifu na matokeo ya utafiti mbalimbali katika kutatua kero za wananchi yanaongezeka kwa kasi kuliko ilivyokuwa huko nyuma.

Mheshimiwa Spika, pamoja na changamoto hiyo upo umuhimu wa kuhakikisha kwamba huduma za Serikali zitolewazo kwa wananchi zinafika kwa haraka na kwa

viwango vinavyotakiwa. Utaratibu wa sasa kila sekta kushughulika na masuala yanayohusu sekta hiyo peke yake lazima urekebishwe kwa kuongeza ushirikiano baina ya sekta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka jana pamoja na kuweka mkazo wa kuongeza ajira inazungumzia sera ya uwezeshaji wananchi kiuchumi. Sera hiyo inalenga katika kuhimiza uchumi na kipato kwa mtu mmoja mmoja, kaya na hatimaye Taifa. Kufanya kazi kwa bidii ndiyo msingi wa sera ya uwezeshaji. Ni vizuri kutambua kwamba ongezeko lolote la kipato cha fedha ni jambo linalomtaka kila mtu mwenye uwezo wa kufanya kazi afanye sasa kwa nguvu, bidii na umahiri mkubwa zaidi. Kila Mtanzania adhamirie kubadilisha hali ya maisha yake aliyo nayo ili sasa yawe mazuri zaidi kwa kuongeza bidii na tija katika eneo la uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, ili kutoa fursa nyingi za uwezeshaji wananchi kiuchumi, Waheshimiwa Wabunge watakumbuka kuwa tumepitisha Miswada miwili inayolenga kuweka mazingira mazuri ya kuvutia wawekezaji wa ndani na nje. Miswada hiyo ni ule wa kufanyia marekebisho Sheria ya Mpango wa Maeneo Maalum ya Uzalishaji kwa Mauzo ya Nje yaani *Export Processing Zones* na Muswada Unaokusudia Kuweka Utaratibu wa Kisheria Utakaosimamia Uanzishaji, Uendeshaji na Usimamizi wa Maeneo Maalum ya Uwekezaji Rasilimali Tanzania Bara. Ni wazi kuwa utekelezaji wa sheria hizi utatuwezesha kuongeza kasi ya kukuza uchumi, kuongeza mauzo nje, kupanua nafasi za ajira na hatimaye kutuwezesha kukabiliana vizuri zaidi na tatizo la umaskini na kuleta maisha bora kwa kila Mtanzania. Hivyo nawahimiza Watanzania kutumia kikamilifu fursa hizi ambazo zitatuwezesha kukabiliana na changamoto za utandawazi.

Mheshimiwa Spika, ili kuongeza kasi ya uwezeshaji wananchi kiuchumi, Serikali itafuatilia kuona kwamba Vyama vya Ushirika Vijijini vinasimamiwa vizuri ili viwe na uwezo wa kununua na kusambaza zana za kilimo, pembejeo na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa vijana wasio na mashamba ni vema Halmashauri ziwatambue na kuwagawia ardhi ili waweze kujiajiri katika kilimo na kuwapatia huduma mbalimbali. Kwa kufanya hivyo, tutakuwa tumeongeza chachu ya wananchi kujitegemea, tutakuwa tumetekeleza Ilani ya CCM ya kuongeza kipato kwa wananchi kuboresha maisha na kuongeza ajira kwa vijana katika eneo la kilimo. Natoa wito kwa Wakuu wa Mikoa na Wilaya kuzingatia jambo hili kwa kutumia mbinu shirikishi na kuzingatia hali halisi.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nizungumzie mambo machache yanayolikabili Taifa letu. Hivi sasa nchi yetu inakabiliwa na tatizo kubwa la ukame na njaa katika maeneo mengi. Kumekuwepo na athari nyingi kutokana na tatizo hili. Tumeeleza hapa Bungeni mkakati na hatua mbalimbali zinazochukuliwa na Serikali kukabiliana na hali hii ambayo ni changamoto kubwa sana kwetu, kwa wananchi na sisi viongozi. Sina mashaka tutavuka janga hili. Hata hivyo, ninachotaka kusisitiza ni uzoefu na mafunzo tunayopata katika kukabiliana na tatizo hili kama Serikali na wananchi wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Serikali, naomba nizishukuru nchi marafiki, Mashirika ya Kimataifa ya ndani na nje ya nchi na watu binafsi ambao wameahidi kutusaidia kukabiliana na tatizo la njaa. Napenda kuwashukuru wale wote ambao tayari wameanza kutoa msaada wa fedha katika Mfuko wa Maafa wa Taifa ili zitumike kununua chakula cha msaada kwa waathirika wa baa njaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuipongeza kipekee Serikali ya Ubelgiji ambayo imetoa msaada wa *Euro 250,000*. Naipongeza Kampuni ya Simu ya *Vodacom* ambayo imetoa msaada wa shilingi bilioni 1. Vile vile nampongeza raia mwema ambaye hakutaka jina lake litajwe ambaye ametoa shilingi milioni 20. Wote hawa nawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue fursa hii kuendelea kuwaomba nchi nyingine marafiki, Mashirika ya Kimataifa ya ndani na nje, Kampuni na wafanyabiashara wengine na watu binafsi ambao watapenda kutoa msaada kusaidia kupunguza athari za baa la njaa. Nimepata simu mbalimbali, tumeelekeza kwamba misaada yote ipelekwe Ofisi ya Waziri Mkuu na itapokelewa na Katibu Mkuu wa Ofisi ya Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mmojawapo ya njia ninayoweza kulihakikishia Taifa usalama wa chakula ni kuhimiza kilimo cha umwagiliaji na utaratibu wa kuhifadhi chakula katika ngazi za kaya. Jamii mbalimbali nchini walikuwa na taratibu zao za kuandaa mabwawa wakati wa kiangazi na kuvuna maji ya mvua ili kuendeleza kilimo cha umwagiliaji. Aidha, zilikuwepo njia za kuhifadhi chakula kwa kutengeneza maghala yao kama vihenge na kutumia taratibu nyingine za asili za hifadhi ya chakula. Pamoja na jitihada mbalimbali zinazofanywa na Serikali kuwasaidia wakulima katika baadhi ya maeneo katika miaka ya hivi karibuni jamii nyingi zimelegalega kutumia taratibu hizo.

Mheshimiwa Spika, wito wangu kwa Watanzania wote ni kuwa tutumie changamoto zilizoko mbele yetu kukabiliana nazo kama daraja lenye kutupa mafunzo ya kuhimiza na kuendeleza taratibu za kisasa na za asili zenye manufaa kwetu. Wakati huo huo, Serikali kwa kushirikiana na wananchi wote itajitahidi kuweka mikakati thabiti ya kuendeleza kilimo cha kisasa kama ilivyotamkwa katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, napenda pia nigusie suala la uharibifu mkubwa wa mazingira uliopo nchini hivi sasa. Upo ukataji miti ovyo sehemu za vilima na katika vyanzo vya maji. Miti imekatwa bila ya kupanda miti mingine. Yapo makundi makubwa ya mifugo inayofugwa bila kujali kama maeneo hayo ni sehemu ya mifugo, ni vyanzo vya maji au ni sehemu ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, yapo matumizi makubwa ya mkaa mabayo ni kiashiria kwamba miti mingi inakatwa kwa ajili ya kuchoma mkaa. Kwa hali hii ni dhahiri kwamba tunahitaji hatua za haraka kuchukuliwa vinginevyo nchi yetu itakuwa jangwa katika muda mfupi ujao.

Mheshimiwa Spika, yapo mambo ambayo uongozi wa Mikoa unaweza kuyafanya bila kungojea maelekezo kutoka ngazi ya Taifa. Mambo hayo yafanyike bila kusubiri. Kwa mfano, vyanzo vya maji vinafahamika, utunzaji wake hauhitaji fedha nyingi ila ujasiri tu wa viongozi katika kuwaelimisha wananchi kupima mipaka ya vyanzo hivyo na kupiga marufuku shughuli zozote za kilimo au mifugo katika maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hifadhi ya maeneo tengefu kama yale yaliyo katika Bonde la Ihefu Mkoani Mbeya ni muhimu Kitaifa. Uongozi wa Mbeya hauwezi tena kukwepa uwajibikaji endapo hawataanza sasa kuchukua hatua za kuhimiza matumizi endelevu ya shughuli za kilimo na mifugo kwenye maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, matatizo tunayoyapata sasa hivi ya umeme ni pamoja na Bonde la Ihefu kukosa maji. Nasema tuko kwenye vita vya kuokoa mazingira yetu. Ni lazima basi mikakati yetu na hatua tunazozichukua ziwe na sura ya uharaka bila kunyanyasa wananchi wala kuvunja sheria na taratibu zilizopo.

Nampongeza sana Waziri wa Maliasili na Utalii na Waziri wa Mazingira kwa sababu wameanza kushughulikia maeneo hayo kikamilifu. Dhamira na melengo yetu yawe ni kurejesha maendeleo yaliyoharibika katika hali yenye uhai katika kipindi kifupi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, elimu ni eneo lingine tunalopashwa kulitazama. Serikali yetu inatambua umuhimu wa elimu na kwamba elimu ni haki ya msingi kwa kila mwananchi. Napenda kusisitiza kuwa kama Taifa tuna jukumu la kuhakikisha kuwa watoto wote waliofaulu darasa la saba mwaka 2005 na ambao walikosa nafasi ya kuingia Sekondari wanapata nafasi angalau nusu yao ifikapo mwezi March, 2006. Kila Mkoa, Wilaya, Tarafa, Kijiji uanze sasa kuchukua hatua kupunguza matatizo hayo. *(Makofi)*

Napenda kulieleza jambo hili kwa takwimu ili sote tutambue ukubwa wa tatizo hilo. Mwaka 2005 wanafunzi 493,946 walifanya mtihani wa darasa la saba. Kati yao wanafunzi 305,062 sawa na asilimia 61.7 walifaulu. Wanafunzi waliopata nafasi katika Shule za Sekondari ni wanafunzi 140,055 tu sawasawa na asilimia 45.9 ya waliofaulu.

Mheshimiwa Spika, hii inamaanisha kwamba jumla ya wananchi 165,007 sawa na asilimia 54.1 walikosa nafasi kuingia Sekondari. Sababu za wanafunzi waliofaulu kukosa nafasi za kuingia Kidato cha Kwanza ni pamoja na ukosefu wa vifaa vya kufundishia, uchache wa shule na madarasa, uhaba wa Walimu, kukosekana kwa nyumba za Walimu na kukosekana kwa motisha kwa Walimu wanaofanya kazi katika mazingira magumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimekutana na viongozi wa Mikoa ya Dar es Salaam na leo Shinyanga na Mbeya ambayo ndiyo iliyofanya vibaya kuliko mingine. Tumekubaliana namna ya kushughulikia tatizo hili. Kwanza nimeagiza kwamba Mikoa yote ambayo asilimia kubwa hawakupata nafasi ya kujiunga na Sekondari wafanye kila jitihada ili

angalau zaidi ya asilimia 50 ya waliofaulu waingie Sekondari mwaka huu kabla ya mwezi March. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili kufanikisha suala hili, Halmashauri ambazo zinapata fedha za maendeleo kuna *Capital Development Grant* na zile zinazopata kutoka *Local Government Development Fund* na *General Purpose Grant* ziangalie uwezekano wa kutumia fedha hizo kujenga madarasa kwa ajili ya kuongeza nafasi zaidi za kusomesha wanafunzi hao. Nashauri utaratibu ufanywe na Halmashauri zinazohusika kufanikisha jambo hili kwa kupanga upya vipaumbele vyao katika Halmashauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa upungufu wa Walimu, utaratibu unafanywa wa kutumia Walimu wastaafu na kutoa mafunzo maalum kwa vijana wanaomaliza Kidato cha Sita ili waweze kusaidia kufundisha kwenye maeneo yaliyo na upungufu wa Walimu. Serikali itaendelea kuongeza nafasi za Walimu ngazi ya Shahada na Stashahada ili kuweza kupata Walimu wa kutosha.

Mheshimiwa Spika, tarehe 11 Februari mwaka huu, Baraza la Mitihani la Taifa lilitangaza matokeo ya Mtihani wa Kidato cha Nne kwa mwaka 2005. Taarifa ya matokeo hayo inaonyesha kwamba kulikuwa na watahiniwa 121,743 kati ya hao watahiniwa waliofaulu katika madaraja 1 mpaka 3 ni 28,653 sawa na asilimia 25.5 ikilinganishwa na watahiniwa 24,520 sawa na asilimia 26.8 waliopata na madaraja hayo mwaka 2004. Hii inaonyesha kuwa kumekuwepo na kushuka kwa kufaulu kwa mwaka 2005 kwa asilimia 1.2 katika madaraja 1 mpaka 3. Matokeo hayo vile vile yanaonyesha kuwa asilimia 83.8 ya watahiniwa wote wamepata madaraja 1 mpaka 4 ikilinganishwa na asilimia 87.1 mwaka 2004 sawa na upungufu wa asilimia 3.3.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla matokeo haya yanaonyesha kuwa shule nyingi za Seminari zinafanya vizuri kuliko shule za Serikali na nyingine. Naomba nitumie nafasi hii kuzipongeza shule hizo na wanafunzi waliofanya vizuri. Lakini kipekee napenda niwapongeze wanafunzi watatu bora wa kike waliofanya vizuri ambao ni Bi. Wende Amani; Bi. Rashida Rashidi na Bi. Dorothea Kashindi wote wa Shule ya St. Francis kule Mbeya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile nawapongeza wanafunzi wa kiume watatu bora Bw. Kado Dambali wa Shule ya Maua Seminari Kilimanjaro; Bwana Ibrahim Shafi na Bwana Hussein Hamidu wote wa Shule ya Sekondari Tanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda pia kutumia nafasi hii kuzipongeza shule tatu bora katika kundi la shule zenye watahiniwa 30 na zaidi. Shule hizo ni *St. Francis Secondary* ya Wasichana, Mbeya, *St. Mary Secondary* Wasichana, Pwani na Maua Seminari, Kilimanjaro. *(Makofi)*

Aidha, napenda kupongeza Shule tatu bora katika kundi la shule zenye watahiniwa chini ya 30 ambazo ni St. Joseph Kiloo Sekondari, Consolata Sekondari na Don Bosco Sekondari zote za Iringa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niruhusu pia nitaje shule 10 zifuatazo ambazo hazikufanya vizuri katika mitihani hiyo. Ndiyo, lazima tuziseme na wasikie kwamba hatukuridhika na walivyofanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, shule hizo zenye watahiniwa 30 na zaidi ni Chemchem Sekondari ya Singida; Yongoe Sekondari ya Pemba; Swai Sekondari ya Tanga; Mbaramo Sekondari ya Tanga; Kitangali Sekondari ya Mtwara; Nyangao Sekondari ya Lindi; Kange Sekondari ya Tanga na Wali Sekondari Kilimanjaro. Wito wangu kwa shule hizi ambazo zina wanafunzi waliofanya vibaya ni kuongeza bidii na waige mifano ya wale waliofanya vizuri.

Mheshimiwa Spika, kwa upande mwingine, matokeo haya yanaonyesha kiwango cha kufaulu kimepungua kidogo ikilinganishwa na mwaka 2004. Ni vema kujiuliza na kujua sababu ya kutofanya vizuri katika matokeo hayo. Zipo sababu mbali mbali za hali hii ikiwa ni pamoja na ongezeko kubwa la wanafunzi ikilinganishwa na upatikanaji wa Walimu wenye sifa na vifaa pamoja na ukosefu wa vivutio kwa Walimu wanaofanya kazi katika mazingira magumu limechangia hali hiyo.

Kwa hiyo, ili kuinua viwango vya kufaulu na ubora wa elimu, Serikali itaongeza idadi na ubora wa Walimu. Itatenga fedha zaidi za kununulia vifaa vya kujifunza na kufundishia na kuongeza madarasa. Vile vile Serikali inaangalia kwa makini kuweka vivutio kwa Walimu wanaofanya kazi katika mazingira magumu ikiwemo posho, ujenzi wa nyumba za Walimu na ajira mpya ya Walimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na hatua hizo, naagiza kila ngazi katika sekta ya elimu kuanzia Shule, Halmashauri, Mkoa na Taifa zifanyike tathmini za kina zitakazobainisha uwezo na udhaifu unaojitokeza katika matokeo hayo na hatimaye kuweka mikakati ya kuboresha elimu ya sekondari. Vile vile nahimiza uwajibikaji, usimamizi na ufuatiliaji wa karibu katika shughuli zote za elimu nchini kwa ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Vyombo vya Habari vinavyotambua wajibu wao kwa jamii ni taasisi muhimu sana hasa katika kipindi hiki. Bado baadhi ya viongozi na hata baadhi ya watendaji Serikalini wanaogopa Vyombo vya Habari. Wananchi wana kiu ya habari, wananchi wana kiu ya elimu, wananchi wana kiu ya kuelewa jinsi kila pembe ya nchi yetu inavyoendelea. Wataweza tu kupata taarifa hizo kwa kupitia Vyombo vya Habari.

Mheshimiwa Spika, ni wajibu wetu tulio ndani ya Serikali na taasisi zake kubadilika. Tuelewe kuwa dhamana tulizo nazo zinatoka kwa wananchi. Kuanzishwa kwa Vitengo vya Elimu na Mawasiliano katika Wizara za Serikali kuendane na dhamira iliyokusudiwa ya kuwawezesha wananchi kuelewa jinsi Serikali yao itakavyotekeleza majukumu yake. Hata hivyo, Vyombo vya Habari navyo vitambue wajibu mkubwa walio nao na mipaka yao katika jamii.

Mheshimiwa Spika, nakubaliana kabisa na pendekezo alilolitoa Mheshimiwa Nyaulawa la kufanya semina maalum kwa Wabunge kwa Waandishi wa Habari wanaoandika shughuli za Bunge ili waweze kuendana na hali halisi ya Bunge bila kupotosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla ya kuhitimisha, napenda kusisitiza mambo yafuatayo. Kwanza, tuweke juhudi zetu zote kuhifadhi mazingira. Suala la mazingira tulifanye kivita.

Mheshimiwa Spika, kila kiongozi kwa nafasi yake asisitize kulinda vyanzo vya maji, kupanda miti msimu wa mvua na kuitunza ili ikue na kila mmoja wetu awe Askari wa kulinda misitu na kuacha kukata miti ovyo. Tujiandaye kufanya zoezi hili na tusisubiri tena kuambiwa.

Pili, tuendelee na mpango wa kujenga madarasa ya sekondari kwa ajili ya watu waliofaulu darasa la saba. Kila Mkoa ambao wanafunzi waliofaulu na kuchaguliwa wako chini ya asilimia 50 wahakikishe angalau asilimia 50 ya wanafunzi hao waliofaulu wanapata nafasi mwaka huu mwezi wa tatu.

Tatu, sisi Wabunge kama viongozi tushirikiane na viongozi wenzetu wa Mikoa, Wilaya na wananchi Majimboni mwetu kuhakikisha kwamba chakula kilichotolewa na Serikali kinawafikia walengwa. Kabla hamjaondoka hapa Dodoma mtapewa nakala ya mgao wa chakula tulichogawa mwezi huu ili mnapokwenda kule Wilayani muweze kujua. *(Makofi)*

Nne, Watanzania tujitahidi kufanya kazi kwa bidii na maarifa na kutumia muda wa kazi kamilifu tukiwa na lengo la kuboresha maisha yetu. Kila mmoja wetu atambue kwamba ana wajibu wa kujiletea maendeleo kwa kufanya kazi kwa bidii. Serikali itakuwa na jukumu la kuwawezesha wananchi wanaojituma kuinua ubora wa maisha yao.

Tano, sisi Wabunge ndiyo kimbilio la wananchi waliotuchagua. Tuwe karibu nao. Tujue matatizo yao. Tushirikiane nao kushughulikia kero zao na maendeleo yao kwa ujumla. Aidha, viongozi wa ngazi zote Serikali waende kwa wananchi kutatua kero zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu swali hapa, naendelea kusisitiza kwamba Mawaziri wa Awamu ya Nne watakuwa mfano kwenda vijijini kushughulika na kero za wananchi na kuzimaliza huko huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii tena kukushukuru wewe mwenyewe na Naibu Spika, kwa kutuongoza kwa busara, kwa hekima na kama ulivyosema mwenyewe, kwa *Speed and Standards. (Makofi)*

Aidha, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa michango yao pamoja na watumishi wote wa Serikali walioisaidia Serikali kujibu maswali na kuwasilisha hoja za Serikali hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mwisho, namshukuru Katibu wa Bunge, Bwana Damian S. L. Foka, pamoja na watumishi wote wa Ofisi ya Bunge kwa kufanikisha Mkutano huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla sijamaliza, naomba na mimi niwapongeze Wabunge tuliowachagua jana kama ifuatavyo:-

Nampongeza Mheshimiwa Kilontsi M. Mporogomyi, kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wetu wa *ACP* na *EU*. *(Makofi)*

Nawapongeza wafuatao ambao wanatuwakilisha katika Chuo Kikuu cha Kilimo. Mheshimiwa Dr. Mzeru O. Nibuka, Mheshimiwa Gaudence C. Kayombo na Mheshimiwa Chacha Z. Wangwe. *(Makofi)*

Nawapongeza wafuatao kwa kuchaguliwa kutuwakilisha katika Chuo Kikuu Huria. Mheshimiwa Beatrice M. Shellukindo, Mheshimiwa Benson M. Mpesya na Mheshimiwa Dr. Ali Tarab Ali. *(Makofi)*

Bunge la *SADC,* nampongeza Naibu Spika, Mheshimiwa Anne S. Makinda, Mheshimiwa Richard S. Nyaulawa, Mheshimiwa *Engineer* Stella M. Manyanya na Mheshimiwa Dr. Wilbrod P. Slaa. *(Makofi)*

Bunge la Afrika, nampongeza Mheshimiwa Omar Sheha Mussa na Mheshimiwa Dr. James M. Wanyancha. *(Makofi)*

Chuo Kikuu Dar es Salaam, nampongeza Mheshimiwa Prof. Raphael B. Mwalyosi; Mheshimiwa Prof. Feethan F. Banyikwa na Mheshimiwa Susana A.J. Lyimo. *(Makofi)*

Chuo Kikuu Mzumbe, nampongeza Mheshimiwa Godfrey W. Zambi. *(Makofi)*

Nawapongeza Waheshimiwa wawili waliochaguliwa kuingia Bunge la Afrika Mashariki, Mheshimiwa Dr. Norman A. Sigalla na Mheshimiwa Hulda S. Kibacha. *(Makofi)*

Tume ya Huduma za Bunge, nawapongeza Waheshimiwa wafuatao. Mheshimiwa Estherina J. Kilasi; Mheshimiwa Philemon Ndesamburo; Mheshimiwa Dr. Chrisant M. Mzindakaya; Mheshimiwa Abdulkarim E.H. Shah na Mheshimiwa William H. Shellukindo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba sasa kutoa hoja kuwa Bunge lako Tukufu liahirishwe sasa hadi siku ya Jumanne tarehe 28 Machi, 2006 saa tatu asubuhi litakapokutana hapa mjini Dodoma.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ni bahati mbaya tu kwamba Kanuni hazimpi nafasi Spika kutoa *Vote of Thanks,* hazinipi nafasi hiyo, basi lakini mniruhusu basi niseme kwamba hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa iliyotoka leo haijawahi kutokea ni ya kihistoria. *(Makofi)*

Hii naiita mimi ni hotuba ya kazi. Tunatoka hapa tunajua watu wanapimwa vipi na watakaopungua basi hayo yatakayowakuta shauri yao. *(Makofi)*

Kabla sijawahoji kuhusu hoja ya kuahirisha Bunge, kuna matangazo. Waheshimiwa Wabunge, mkumbuke kesho tunayo semina ya *TACAIDS* ambayo inafanya tathmini ya hali halisi ya ugonjwa wa UKIMWI katika nchi yetu mpaka sasa yaani tathmini na njia ambazo sasa au mipango itakayokuwepo ya kuendelea kudhibiti gonjwa hili. Semina ni saa tatu asubuhi hapa hapa katika ukumbi huu hadi saa sita na nusu. Mnaombwa sana tuhudhurie ili tuweze kuona na kusikia yale ambayo yanaisibu nchi yetu kwa gonjwa hili.

La pili, ni kwamba Waheshimiwa Wabunge wa Chama cha *APNAC* wanaombwa kukutana, ukumbi umetajwa tena ule wa 231, naona watasikilizana na wenzao waliotangulia mara baada ya Kuahirisha Bunge. Nadhani wanajifahamu.

Baada ya kusema hayo, Waheshimiwa Wabunge Hoja ya Kuahirisha Bunge iko mbele yetu. Kwa hiyo, naliahirisha Bunge hadi siku ya Jumanne, tarehe 28 Machi, 2006 saa tatu asubuhi hapa Dodoma. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Saa 05.27 Asubuhi Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Jumanne, Tarehe 28 Machi, 2006 saa tatu asubuhi)*